Mtangazaji Gadner Habash afariki dunia



UK. 4


**Nchimbi** ataka wananchi kuchangamkia mikopo 10%

UKURASA 8



**Makonda** ageukia dawa za kulevya

UKURASA 2




UKURASA 14

Jumapili Aprili 21, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581653

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Hatima kikokotoo kujulikana Mei Mosi

UKURASA 2



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, akizungumza Bungeni Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

MSEMAJI MKUU WA SERIKALI

## Mafuriko yameathiri zaidi ya wananchi 200,000

UKURASA 4




MIAKA 60 YA MUUNGANO

OFA KATIKA TOLEO MAALUM!!

Katika kuadhimisha Siku ya Muungano mwaka huu, tarehe 26 April 2024 Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian Itatoa toleo maalum la Muungano, hivyo inawakaribisha kutoa salamu za kumbukizi, matangazo, picha na makala za mafanikio katika kusherekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa PUNGUZO MAALUM

Wahi mapema kwa sikukuu hii upate PUNGUZO, Artwork ya bure na nafasi katika majukwaa yetu ya kidigitali.

*vigezo na masharti kuzingatiwa*

The Guardian | Nipashe

KWA MAWASILIANO TUPIGIE | +255 677 020 701

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz Au Tutembelee The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Mkabala na ITV / Radio One, Dar es Salaam
Tovuti: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

RIPOTI CAG

UKURASA 3

## ACT walia upigaji Tril. 3/- serikalini

MICHEZO YANGA YAENDELEZA UBABE KWA SIMBA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Makonda aanza kupambana dawa za kulevya Arusha

**Na Beatrice Shayo**

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha, limetakiwa kutatua changamoto za matukio ya uhalifu, rushwa na dawa za kulevya na kuhakikisha yanakuwa historia mkoani humo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, alipokuwa akizungumza kwenye kikao kazi kilichohusisha uongozi wa Jeshi la Polisi mkoani humo.

Makonda alisema Jeshi la Polisi linapaswa kufahamu taarifa za kuwapo wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya mkoani humo haileti taswira nzuri kwa kuwa mkoa huo unapaswa kuwa kitovu cha kuzungumzwa kwa mazuri kutokana na rasilimali zilizoko na wanaweza kutengeneza hofu kwa baadhi ya wageni kuingia na kufanya biashara.

Alisema vita ya dawa za kulevya haijawahi kuwa nyepesi, maofisa wa Jeshi la Polisi mkoani humo wanatakiwa kujipanga kikamilifu kuhakikisha wanaishinda.

Akizungumzia masuala ya rushwa, Makonda aliwataka askari na maofisa wa polisi mkoani humo kujitengenezea taswira njema kwa jamii kwa kuwa, haipendezi na haikubaliki kuona askari mmoja anapokea mlungula.

Alimuagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, kusimamia nidhamu na weledi kwa jicho kali inapotokea askari mmoja au kituo kimoja kinalalamikiwa kwa rushwa na matendo mengine yasiyofaa.

Ametaka hatua stahiki zichukuliwe kwa haraka kwa kuwa, mafanikio ya mpokea rushwa ni laana inayoathiri watoto na familia.

Aliwataka maofisa hao kutambua wana wajibu wa kutoa huduma nzuri kwa wananchi na matarajio ni kuona Jeshi la Polisi mkoani humo linakuwa la mfano kwa weledi, nidhamu na uwajibikaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, ACP Justine Masejo, alisema miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni upungufu wa vyombo vya usafiri ikiwamo pikipiki zitakazowasaidia polisi kata kutimiza majukumu yao ya kila siku ya kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarika katika kata zao.

Kamanda Masejo alisema licha ya kuwa na kitengo maalum cha polisi wa utalii na diplomasia, ni vyema wangepatiwa gari maalumu litakalotumika kusaidia kuongoza misafara ya watalii kutoka uwanja wa ndege hadi kwenye maeneo ya hifadhi au hotelini.

Alisema mara zote jeshi hilo mkoani humo limekuwa kinara wa kusimamia nidhamu kwa watumishi wake na maofisa wa polisi wanaokwenda kinyume na taratibu za jeshi, wanachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufukuzwa kazi, jambo aliloahidi kuwa ni endelevu.

Kamanda Masejo ameahidi kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, biashara haramu ya dawa za kulevya na uhalifu mwingine.




Mwananchi akiangalia pikipiki iliyogongwa na gari ya abiria inayofanya safari zake kati ya Mabibo na Mnazi Mmoja katika eneo la Msimbazi Center jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hatima kikokotoo Mei Mosi

**Na Vitus Audax,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, amesema suala la kanuni mpya ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu litajulikana Mei Mosi, Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge juzi bungeni jijini Dodoma, Katambi alisema serikali haiwezi kufumbia macho wala masikio suala hilo.

Alisema licha ya maelezo mbalimbali yanayotolewa ndani na nje ya Bunge, suala hilo linatarajiwa kutolewa majibu na Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi, yakakayofanyika jijini Arusha.

"Rais ameshatoa maelekezo zaidi ya mara mbili kwamba tulifanyie mapitio upya kuona namna ya kukifanyia maboresho zaidi ili wastaafu wasipate shida, tayari tumeanza kazi hiyo na sheria inatutaka kufanyia maboresho kila baada ya miaka mitatu na tayari imepita.

"Tunaendelea kulifanyia kazi maana tumepokea maelekezo ya Rais pamoja na Bunge, lakini pengine tunaweza kusikia kauli ya Rais katika viwanja vya Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Siku ya Mei Mosi atakapokutana na wafanyakazi kueleza suala hili, hivyo tumelipa uzito unaostahili kuhakikisha tunaliweka sawa," alisema.

**ULIPAJI MISHAHARA**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema wizara yake ipo katika mabadiliko makubwa yanayolenga kuwanufaisha na kuwainua watumishi wote katika nyanja mbalimbali.

Wakati akihitimisha hoja za wabunge na Bunge kuidhinishia wizara hiyo Sh. trilioni 1.10 kwa mwaka 2024/25, Simbachawene alisema kwa sasa hakutakuwa tena na malimbikizo ya mishahara, kwa kuwa fedha kwa ajili ya ulipaji zinatolewa kila mwaka.

Alisema kwa mwaka 2023/24, ilichukua fedha ya bajeti ya serikali ya Sh. bilioni 153.9 na kwa mwaka 2024/25 zimeombwa Sh. bilioni 150.8 na kuwa, hali itaendelea kwa utaratibu huo kila mwaka, kwa kuwa lengo la Rais Samia ni kila mtu apate anachostahili bila kudhulumiwa haki yake.

Pia, alisema serikali inaendelea kulipa malimbikizo ya mishahara na watumishi 26,331 wamehakikishiwa kulipwa zaidi ya Sh. bilioni 39.55.

Kuhusu upandishaji vyeo, Simbachawene alisema serikali imerejesha utaratibu wa kupandisha vyeo watumishi kila baada ya miaka mitatu tofauti na awali ilikuwa ni baada ya miaka minne.

Alisema Rais Samia ameridhia kupandisha vyeo watumishi 81,515 waliokasimiwa katika bajeti ya mwaka 2023/24 kwa gharama ya Sh. bilioni 130.47.

Vilevile, serikali imepanga kuwapandisha vyeo watumishi 219,924 waliokasimiwa katika bajeti ya 2024/25, kwa gharama ya Sh. bilioni 252.7 na kufanya idadi hiyo kufikia 301,439, kwa miaka miwili ya fedha.

Alisema serikali imelipa mishahara kwa wafanyakazi wa mamlaka za serikali za mitaa 113 zenye jumla ya watumishi 691 kwa awamu.

Awamu ya kwanza, serikali imetenga Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya kugharamia mishahara ya watumishi 474 wa mamlaka za serikali za mitaa 101 ambazo zimebainika kuwa na uwezo mdogo kutokana na kushindwa kuwalipa.

"Nisisitize madeni ya watumishi hawa ambayo wanadai mamlaka hizo, ziwalipe na sisi tutaanza kuchukua hatua kwa wakurugenzi ambao tunapeleka maelekezo ya kulipa stahiki za madeni yanayotokana na watumishi walio chini yao halafu hawafanyi hivyo, hatua za kisheria tutazichukua kwa njia za kiutumishi," alisema.

Alisema hiyo ni kutokana na kuwa kama mchezo, kwani watumishi wanalalamika maelekezo yanatolewa kwa mkurugenzi, lakini hawataki kuwalipa, hivyo kuahidi kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Waziri Simbachawene alisema baadhi ya maeneo nchini yana upungufu wa watumishi, huku mengine yakiwa na watumishi wengi kupita kiasi, waking'ang'ania yenye mazingira mazuri na kuacha maeneo ya pembezoni.

Serikali imeamua baada ya majadiliano ya wizara tatu za Utumishi, TAMISEMI na Fedha, baada ya bajeti hiyo watahakikisha wanafanya mgawanyo wa walimu nchi nzima.

"Naomba niseme hapa, tusirudi tena hapa kulalamika kwa kuwa tutakapoanza operesheni hii haitamuacha mtu na wala haitakuwa na upendeleo, lakini tutazingatia hali na sababu mahususi walizonazo watumishi wetu," alisema.

"Katika kutekeleza hili pia, lipo suala limeibuka la wenza na kwa kuwa mwajiri ni serikali na inahimiza maadili, hivyo tutahakikisha kila mwenye mwenza wake wa kweli wanakwenda kufanya kazi katika eneo moja hata kama siyo kituo kimoja," alisisitiza.

**UMILIKI NDEGE ATCL**

Kuhusu kuhamisha umiliki wa ndege kutoka Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania (TGFA) kwenda Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), alisema ni hoja inayoibuka mara kwa mara, lakini tayari limejadiliwa na utekelezaji unaendelea.

"Tunatambua kwa sasa ATCL inafanyakazi nzuri na tayari tulishakaa kamati kuhusu suala hili na utaratibu unaendelea, lakini tutambue kuhamisha ndege sio suala la haraka kiasi hicho, hivyo kuna michakato yake ya kimataifa na pia kitaifa inayoendelea," alisema Simbachawene.

**USAILI KIDIJITALI**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema tayari serikali imetatua kero ya watu kusafiri kutoka mikoani kwenda Dodoma kufanya usaili kwa ajili ya ajira mpya.

Alisema kutokana na malalamiko kuhusu watu wanaoomba fursa za ajira kulazimika kufunga safari na kutumia gharama kubwa kwenda Dodoma kufanya usaili, ufumbuzi wake umepatikana na sasa utafanyika kwa njia ya kijitali.

Pia, wizara hiyo imeanza usaili kidijitali kupitia mfumo wa 'Online Aptitude Test System'.

"Mara ya kwanza ulitumika kufanyia usaili Tanzania nzima na kwa siku hiyo, kwa mara ya kwanza hatukupata malalamiko lolote kuhusu utaratibu huu," alisema Ridhiwani.

Alisema malengo ya serikali baada ya kuonekana kuwa umefanikiwa ni kuhakikisha taratibu nyingine za usaili katika kada zote unafanyika kupitia mfumo huo ili kufanyika maeneo yao.

"Nataka niwahakikishie sasa kwa wale wanaotoka katika mikoa ya mbali na Dodoma wakiwamo wa upande wa visiwani, sasa wataweza kufanya usaili wakiwa katika maeneo yao," alisema.

HABARI KITAIFA

# ACT walia upigaji tril 3/- serikalini

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimechambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23, kikitaka hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watendaji wa serikali wanaonyooshewa kidole kufanya ubadhirifu wa jumla ya Sh. trilioni 3.14.

Dorothy Semu, Kiongozi wa ACT Wazalendo, wakati wa kuwasilisha uchambuzi huo kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema wamechagua maeneo 10 waliyoona ni muhimu zaidi Watanzania kuyatambua na wameyatolea mapendekezo ili yafanyiwe kazi, ikiwamo hoja hiyo ya ubadhirifu wa fedha za umma.

Alisema uchambuzi wao umebaini CAG ameibua hoja nyingi zinazopaswa kufanyiwa kazi. Baadhi ya hoja hizo zitazingatiwa kwenye uchambuzi wa bajeti wa kila wizara ya serikali utakaofanywa na wasemaji wao wa kisekta.

Waziri Kivuli wa Fedha, Mipango na Hifadhi ya Jamii wa chama hicho, Kizza Mayeye, alisema ripoti hiyo ya CAG imeendelea kuonesha uzembe unaofanywa na serikali uliosababisha upotevu wa makusanyo na mapato katika wizara, idara na taasisi za serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, miradi ya maendeleo na mashirika ya umma.

Alisema wameona kwa mara nyingine vitendo au uamuzi wenye viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma katika utekelezaji miradi na majukumu mbalimbali ya wizara na taasisi za serikali kukiwa na hoja za ubadhirifu na upotevu wa fedha za makusanyo zenye jumla ya Sh. trilioni 3.14.

Alifafanua kuwa katika fedha hizo, halmashauri zimeonesha upotevu wa Sh. bilioni 167.8, wizara, idara na taasisi za serikali zina upotevu wenye thamani ya Sh. bilioni 103.32, gharama zinazotokana na ucheleweshaji kutelekezwa kwa miradi ya maendeleo zina jumla ya Sh. bilioni 744.1, dosari za kiusanifu za Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwenye miradi ya barabara sita Sh. bilioni 130.51, mradi wa BRT Sh. bilioni 28.05, Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere Sh. bilioni 327 na mashirika ya umma yana hoja zenye thamani ya Sh. trilioni 2.23.

"Taarifa ya CAG inathibitisha tena tatizo sugu la serikali kuendelea kupoteza na kutumia vibaya fedha za umma bila hatua za uwajibishaji kuchukuliwa. ACT Wazalendo tunataka watu wote waliohusika na ubadhirifu na uzembe uliopelekea upotevu wa fedha za umma wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria," Kizza alipendekeza.




Waziri Mkuu Kivuli wa Chama cha ACT-Wazalendo, Isihaka Mchinjita, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla ya uchambuzi wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

Waziri Kivuli huyo pia alizungumzia dosari ya fedha kutopitishwa Mfuko Mkuu wa Hazina, akiitaja ni mwanya wa ufisadi.

Alisema kuwa uchambuzi wao umebaini kuwa kwa mwaka 2022/23, jumla ya matumizi yenye thamani ya Sh. trilioni 3.2 yalifanywa bila kupita Mfuko Mkuu wa Serikali, sehemu kubwa ya fedha hizo inatokana na fedha zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi kutoka kwa wadau wa maendeleo.

"Fedha hizi za miradi zinaonekana katika vitabu vya bajeti, lakini CAG hazioni kuingia Mfuko Mkuu na hivyo kutoka kwake ni kinyume cha sheria. Matumizi ya aina hii licha ya kuwa ni kinyume cha katiba na sheria za nchi, huwa ni kichaka cha kuficha ubadhirifu kwani kutumia fedha namna hii kunamnyima CAG kufanya kazi yake ya udhibiti wa fedha za umma," alihadharisha.

Waziri Kivuli huyo pia alisema CAG katika ripoti ya ufanisi wa usimamizi wa shughuli za kilimo, ameonesha wakulima wengi nchini hawajapata mbolea zenye ruzuku licha ya serikali kutenga wastani wa Sh. bilioni 150 kila mwaka.

Alisema CAG ameonesha kuwa wakulima milioni 2.55 kati ya milioni 3.4 waliosajiliwa katika mpango wa ruzuku (sawa na asilimia 75) hawakupata wala kutumia mbolea kupitia mpango wa ruzuku licha ya kuwa na sifa ya kupata mbolea hiyo ya ruzuku kwa mwaka huo wa ukaguzi.

### UAGIZAJI PETROLI

Kizza pia alisema uchambuzi wao umegusa dosari katika uagizaji, uingizaji na usambazaji wa mafuta nchini, akiitaja ndiyo kiini cha kupanda kwa gharama ya mafuta nchini.

Alisema imebaini nchi haina Hifadhi ya Taifa ya Petroli, CAG akionesha kama Taifa kukosa hifadhi ya petroli ya mkakati kunaiweka nchi katika hatari ya kuwa na uhaba wa nishati wakati wa shida.

Vilevile alisema nchi ina uwezo mdogo wa miundombinu mafuta, CAG akionesha kuna bomba moja tu linalotumika kuingiza mafuta Tanga, Mtwara na Dar es Salaam na bomba hilo moja ndilo hutumika kusafirisha petroli na dizeli, baada ya kusafirisha petroli linasafishwa ili kupitishwa dizeli.

"Bomba hili limetumika kuanzia 2012 ambapo lilitumika kusafirishia Metric Tone 250,000, sasa linapitisha 650,000. Serikali ya CCM inafanya mchezo na suala hili nyeti, sisi tunaona ni lazima kuweka mkazo mkubwa sana kwenye eneo hili hasa ukizingatia mambo kadhaa yanaweza kuteteresha usambazaji wa mafuta duniani kama vile migogoro ya kieneo (vita Mashariki ya Kati), majanga, vikwazo vya kiuchumi kwa baadhi ya nchi," alisema.

### DENI LA SERIKALI

Waziri Kivuli huyo pia alizungumzia hoja ya kasi ya ukuaji wa Deni la Serikali na hatari zake kwa taifa, akisema CAG ameonesha ukuaji wa kasi wa deni hilo. Hadi Juni 30, 2023, Deni la Serikali lilikuwa Sh. trilioni 82.25 sawa na Ongezeko Sh. trilioni 10.94 (asilimia 15) kutoka mwaka wa fedha uliotangulia (2021/22).

"Uchambuzi wetu wa CAG kuhusu mwenendo wa Deni la Serikali ni kuwa kasi ya ukuaji wa Deni la Serikali inatishia maendeleo ya watu, uwezo wa nchi kujihudumia na kusababisha ukuaji wa uchumi unaoendeshwa na deni (debt driven growth)," alisema.

### MIFUKO HIFADHI YA JAMII

Madai ya wafanyakazi Sh. bilioni 36.47 na michango yao (sh. bilioni 856.78 kutowasilishwa kwenye Mifuko ya hifadhi ya Jamii.

Kiongozi wa Chama hicho, Dorothy, alizungumzia hoja madai ya wafanyakazi Sh. bilioni 36.47 na michango yao Sh. bilioni 856.78 kutowasilishwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alisema ripoti ya CAG kwa mwaka 2022/23 imeonesha madai ya Sh. bilioni 36.47 ya watumishi wa umma katika halmashauri 54. Madai hayo yanajumuisha malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi, stahiki za wastaafu na posho za kisheria.

"Kutokulipwa kwa madai haya kunaongeza ugumu wa maisha kwa wafanyakazi ikizingatia tayari gharama za bidhaa muhimu zinaendelea kupanda kila uchao.

Pia ni kinyume cha kanuni ya utumishi wa umma inayoelekeza mfanyakazi yeyote wa serikali pale anapopandishwa daraja au kuteuliwa kwenye nafasi ya kiwango cha juu, alipwe malipo ya nyongeza ya mshahara yanayostahili.

"ACT Wazalendo tunaitaka na serikali na waajiri binafsi kuheshimu matakwa ya sheria ya mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kuwasilisha kwa wakati michango ya wafanyakazi. Pia tunaitaka serikali kulipa malimbikizo ya madai yote ya watumishi na wastaafu," alisema.

### MADUDU MWENDOKASI

Waziri Mkuu Kivuli na Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Tanzania Bara, Isihaka Mchinjita alizungumzia hoja ya usimamizi mbovu wa mradi wa mabasi yaendayo haraka, maarufu mwendokasi.

Alisema CAG amebaini kuna usimamizi mbovu kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ambao upo chini ya OR-TAMISEMI. Mradi wa Sh. bilioni 217.48 wa kutoka Katikati ya Jiji hadi Mbagala umekamilika kwa asilimia 98.86 lakini hautoi huduma.

Vilevile, alisma DART wamekalia bidhaa za Sh. bilioni 3.43 za mifumo ya kukusanya nauli, CAG akionesha kuwa DART ilinunua kadi janja za Sh. bilioni moja na mifumo mingine ya TEHAMA ya kukusanyia nauli ya Sh. bilioni 2.43 vimetelekezwa.

"Pia kuna utoaji huduma usioridhisha. CAG ameonesha kati ya mabasi 210 ya mkataba, mabasi 132 (asilimia 63) yalikuwa mabovu na hayatoi huduma na kwamba yanahitaji Sh. bilioni 2.1 za matengenezo, lakini hazijatolewa. Yapo yanaoza, wanakimbilia kutoa zabuni kwa mwekezaji kutoka nje.

"Hoja zote alizotoa CAG ni hoja zinazotokana na uzembe wa kiutendaji na kimenejimenti na zina harufu ya uhujumu uchumi. Hii inasababisha kukosekana kwa thamani halisi ya fedha na kutotatua tatizo la usafiri jijini Dar es Salaam," alisema.

"ACT Wazalendo tunapendekeza Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI ajiuzulu kwa kushindwa kuisimamia DART na kusababisha hasara kubwa kwa Taifa. Pia Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI pamoja na bodi ya wakurugenzi wa DART na wahusika wengine wote wafikishwe mahakamani kwa makosa ya kuhujumu uchumi," alisema.

Waziri Mkuu Kivuli huyo alizungumzia Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP), akigusia kutotolewa fedha za uwajibikaji kwa jamii (CSR) Sh. bilioni 270 (asilimia tatu ya fedha za mradi).

Chama hicho pia kimeitaka serikali kulipa Sh. bilioni 208 za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ambazo ilizichukua kama mkopo tangu mwaka 2020. Kimebainisha kuwa CAG pia ameonesha kuwa hadi kufikia 30 Juni 2023, NHIF imekusanya Sh. bilioni 5.6 (12.6%) pekee kati ya Sh. bilioni 42.57 inazozidai taasisi za serikali na binafsi ikiwa ni michango ya wanachama.

Kati yake, michango ambayo zinadaiwa taasisi za serikali ni Sh. bilioni 19.04 (45%) na Sh. bilioni 23.53 (55%) zinajumuisha madeni kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali.

Chama hicho pia kimeitaka serikali imilikishe Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ndege zote inazokodishiwa na kurejesha Wakala wa Ndege (TGFA) chini ya Wizara ya Uchukuzi kutoka Ofisi ya Rais.

Pia kimemtaka CAG kufanya ukaguzi maalum wa ununuzi wa ndege tangu ulipoanza mwaka 2016 hadi sasa.




Daktari wa Hospitali ya Tiba Healthcare, Jamil Suleiman, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu kampuni ya Skechers kuleta viatu maalum vya tiba ambavyo hutibu maradhi mbalimbali ya miguu na mgongo, Kushoto ni Meneja Masoko wa kampuni ya Skechers, Micky Decha.**PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wananchi 273,159 waathiriwa na mafuriko

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema wananchi 273,159 hawana makazi kutokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini.

Kadhalika, viongozi wa dini wataondoka leo na treni ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam kuelekea Dodoma kwa ajili ya kufanya maombi na dua ya kuliombea taifa kesho.

Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), Mobhare Matinyi, alisema jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alikuwa akizungumzia mafuriko, Muungano na safari ya majaribio ya treni ya kisasa (SGR).

Alisema idadi ya walioathirika kwa Mkoa wa Pwani ni

kaya 29,510 watu 125,668, Morogoro kaya 12,824 watu 51,491 na Mbeya kaya 27, 000 watu 96,000.

Katika maeneo ya Rufiji mafuriko yameanza kupungua kutokana na mvua kupungua katika baadhi ya mikoa ambayo mito yake huingiza maji katika Bonde la Rufiji.

Matinyi alisema kutokana na athari hizo za mvua walianzisha makazi ya muda na hadi sasa kuna kambi sita zenye waathirika 2,883 kwa Mkoa wa Pwani yenye kaya 29,510 zilizoathirika.

Alisema mvua hiyo imeathiri miundombinu ya barabara, vituo vya afya, shule, nyumba, mifumo ya maji na mashamba 152,956. 24 yenye mazao ya chakula.

Aidha, alisema misaada inaendelea kupelekwa katika mikoa ya Pwani, tani 700 za chakula, mafuta ya kula lita 7,880, vyandarua 2,260, mablanketi 1,290 na vifaa vingine ikiwamo mahema 26, magodoro 1,258, mafuta ya petroli lita 3,000 na dizeli 2,900.

Matinyi alisema mahitaji mengine kwa Mkoa wa Pwani ni boti mbili zaidi, umeme wa nguvu za jua, magodoro 2,000, vitanda 150, matangi 50 ya lita 5,000, mahema makubwa manne na madogo 10, mafuta ya petroli lita 100,000 na dizeli 50,000.

"Misaada inaendelea kuja na wahisani wanaombwa kuelekeza misaada Wilaya ya Kibiti ambapo hadi sasa kumekuwa na uhaba wa misaada kutokana na mingi kupelekwa Rufiji," alisema Matinyi.

Alisema kwa Mkoa wa Morogoro kuna jumla ya kata 50 zilizoathirika na mafuriko na watu 78 waliokolewa na serikali. Sasa kuna kambi sita za waathirika zenye watu 1,500 na Mlimba kuna waathirika 1,365, Ifakara 135 zilizopo halmashauri mbili za Wilaya ya Kilombero.

Alisema watu wote waliopata mafuriko wapo katika makambi wanahudumiwa na serikali kwa kupewa chakula, makazi, tiba, maji na usalama.

Matinyi alisema tathimini ya mafuriko ya mvua inaendelea kufanywa na watatoa taarifa ikiwamo idadi kamili ya vifo vilivyotokana na mafuriko ya mvua.

Aidha, alisema viongozi wa dini, watendaji wa serikali, watumishi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na waandishi wa habari baada ya kumaliza ibada kesho watapanda treni hiyo majira ya saa nane mchana na kuwasili Dar es Salaam majira ya saa moja usiku.

Alisema treni hiyo ipo katika majaribio, na isije kuonekana imetumia muda mrefu kusafiri. "Hizi ni shughuli za majaribio mwendokasi sio kipimo cha kazi haya ni majaribio."

Alisema hadi sasa wameshapokea mabehewa ya treni ya kisasa 65 na vichwa tisa "kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro kimekamilika kwa asilimia 98.9 na kipande cha Morogoro kwenda Dodoma kimekamilika kwa asilimia 96.1."

Alisema nchi inaadhimisha miaka 60 ya Muungano na kumekuwa na matukio mbalimbali ya kuzindua miradi, tukio kubwa linalofuata Aprili 22, mwaka huu jijini Dodoma ni kuliombea taifa na mgeni rasmi ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema wananchi wataanza kuingia katika uwanja kuanzia saa 12 asubuhi kutakuwa na burudani mbalimbali ikiwamo kwaya na shughuli la kuliombea taifa itaongozwa na viongozi wa dini.

Alisema tukio jingine kubwa ni Aprili 24, mwa huu kutakuwa na uzinduzi wa kitabu cha miaka 60 ya historia ya Makamu wa Rais iliyoanzishwa baada ya Muungano kutokea.

Aidha, alisema Aprili 25, majira ya saa tatu Rais Samia Suluhu Hassan, atalihutubia taifa kutoa ujumbe wa maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano saa sita kamili usiku, mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Geita, Mbeya, Mwanza na Zanzibar kutakuwa na urushwaji wa fataki.

Alisema Aprili 26, kilele cha shughuli hizo zitafanyika katika kiwanja cha Uhuru na mgeni rasmi atakuwa Rais Samia.

Taifa linatarajia kuwa na wageni kutoka mataifa ya jirani na marafiki katika siku hiyo.

# Mtangazaji Clouds FM Gardner Habash afariki, aliliwa kila kona

**Na Romana Mallya**

MTANGAZAJI nguli wa kipindi cha Jahazi, Kituo cha Redio cha Clouds FM, Gardner G. Habash, maarufu Captain amefariki dunia jana asubuhi katika Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), wakati akiendelea na matibabu.

Msemaji wa Kampuni ya Clouds Media Group, Emilian Mallya, alisema msiba upo nyumbani kwa marehemu maeneo ya Kijitonyama karibu na Kituo cha Polisi Mabatini.

Gargner alijipatia umaarufu mkubwa kutokana na ucheshi na aina ya utangazaji wake katika kipindi cha Jahazi na hadi umauti unamkuta, mtangazaji huyo alikuwa amelazwa katika Taasisi hiyo kutokana na maradhi ya shinikizo la damu.

Katika mahojiano yake na kipindi cha XXL yaliyofanyika mwanzoni mwa mwezi huu, Gardner alisema alianza kujisikia vibaya wiki chache zilizopita baadaye akapelekwa hospitalini ambako aligundulika kuwa na shida ambayo ililazimika kulazwa.

Machi 17, mwaka huu, binti yake ambaye ni msanii wa Bongo Flava, Malkia Karen, alitupia picha katika ukurasa wake wa Instagram akiwa na baba yake (Gardner) na mtoto wake (mjukuu wa mtangazaji huyo), wakiwa katika moja ya hoteli akimtakia kheri ya siku yake ya kuzaliwa akitimiza miaka 50. Baadhi ya watu maarufu wakiwamo viongozi wa serikali, wanasiasa na wasanii, muda mfupi baada ya taarifa hiyo, katika kurasa zao waliweka picha ya mtangazaji huyo akiwa kazini enzi za uhai wake kama sehemu ya kuomboleza kifo chake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, katika ukurasa wake wa Instagram aliandika, "Nimeshtushwa. Nimeumia na nimesikitishwa sana na kifo cha kaka Gardner G. Habash, mtangazaji mwandamizi wa vyombo vya habari Clouds.

"Lala salama bro (kaka), umefanya mengi katika tasnia yetu ya habari. Mwendo umeumaliza, huna baya. Poleni wanafamilia, Clouds Media, ndugu, jamaa na marafiki." Aliyewahi kuwa Mbunge wa Mikumi (CHADEMA), Joseph Haule na msanii wa Hip Hop, Profesa Jay aliandika, "Pumzika kwa amani ndugu yangu Captain, tangulia na sisi tunafuatia kaka.

"Poleni sana Malkia Karen, Clouds Media Group pamoja na ndugu, jamaa na marafiki cha msingi, tumuombee ndugu yetu alale salama." Msanii wa Bongo Flava, Nandy aliandika, "Daah! Kaka yangu pumzika kwa amani wewe ni moja ya mtu poa sana support (msaada) yako itaishi mioyoni mwetu. Rest in peace brother (pumzika kwa amani kaka)."

Zamaradi Mketema katika ukurasa wake wa Instagram aliandika, "Aaah Gadna jamani, Inalillahi waina Ilaihi Rajiun. Mungu akupumpishe kwa amani kaka, Dah! Pumzika kwa amani kaka. Kazi ya Mungu haina makosa."

Alianzia Kituo cha Redio cha Clouds DM, akaenda Times FM na kisha kurejea Clouds FM hadi umauti unamkuta, Gardner pumzika kwa amani.

HABARI KITAIFA

# W'biashara Soko la Coca-Cola walivyodhibiti uhalifu

**Na Mary Geofrey**

WAMACHINGA wa soko la Coca-Cola Mwenge, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, wamefanikiwa kudhibiti makundi ya wahalifu waliokuwa wanajificha sokoni. Makundi hayo ni wezi wanaovunja na kuiba katika nyumba za watu, wanaopora mali, wauzaji na wavutaji wa bangi, wanaojisaidia barabarani na wanaodhalilisha wanawake na wasichana kwa kuwatomasa bila ridhaa.

Katika taarifa ya Mwenyekiti wa soko hilo, Abdallah Samata, aliyoitoa juzi kwa vyombo vya habari, ilisema kutokana na kukithiri vitendo hivyo walilazimika kuchukua hatua za kufanya ulinzi shirikishi kuanzia mwezi Januari, mwaka huu.

"Sasa hivi ukipita soko la Coca-Cola Mwenge hutaamini unachokiona, ukiacha simu unaikuta, hakuna wavuta bangi, hakuna wanaopapasa wasichana au wanafunzi," alisema Samata.

Aidha, alisema kabla ya kutangaza uamuzi huo walitoa taarifa katika Ofisi za Serikali ya Mtaa, kata na vituo vyote vya polisi kwa kupeleka barua ili kupata ridhaa hiyo.

"Viongozi wa serikali za mtaa, wilaya na Mkoa wa Dar es Salaam walitusikiliza na kuelewa nia yetu njema na kutuunga mkono katika kumaliza haya makundi. Walifika katika eneo letu la soko na kushuhudia hali halisi ya uharibifu, mmomonyoko wa maadili na uhalifu unaofanywa na baadhi ya watu," alisema Samata.

Kadhalika, uongozi wa soko kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walichukua hatua zinazoendelea ili kuliweka eneo la machinga pamoja na viunga vyake kuwa salama kwa wafanyabishara na watumiaji wote.

Kiongozi huyo aliwasihi wafanyabiashara wa masoko mengine kuiga mfano huo kwa kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo yote ya biashara na kuondokana na dhana kuwa maeneo ya soko kutumika kuwa makazi ya wahalifu.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya Simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Mtatiro Kitinkwi, alisema operesheni hiyo imesaidia kumaliza wahalifu katika eneo hilo. Alisema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na wafanyabishara wa eneo hilo na kutoa rai kwa maeneo mengine kushirikiana ili kumaliza uhalifu na wahalifu katika mitaa na maeneo yao.



Mfanyabiashara wa mihogo akiipanga kuvutia wateja kandokando mwa barabara ya Chanika Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge ataka umiliki wa ndege uwe chini ya ATCL

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Mlalo (CCM), Rashid Shangazi, (CCM) ameitaka serikali kuondoa umiliki wa ndege katika Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania (TGFA) na kuwekwa chini ya usimamizi wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ili kuondoa utaratibu wa serikali kujikodishia mali zake yenyewe na kushindwa kulipa.

Shangazi alitoa kauli hiyo juzi wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2024/25.

Alisema hatua ya TGFA kulikodisha ATCL ndege ambazo zinasomeka kama mali za serikali moja kwa moja, licha ya serikali kuingia kwenye madeni makubwa ya yenyewe kwa yenyewe, pia imekuwa ikisababisha ndege hizo kukamatwa nje na wadai wa serikali.

"Sasa unapokodisha ndege imenunuliwa na serikali kwa shirika la serikali. Hapa cha kutazama ni kuwa ndege ya serikali inapokuwa kwenye wakala wa serikali deni linakuwa ni la serikali, hali inayofanya ndege hizo zikamatwe.

"Tumeishakamatiwa ndege hapa hivi karibuni na nyinyi ni mashahidi kwa sababu, ndege zinasoma kuwa ni mali ya serikali, lakini zingekuwa za ATCL, ingekuwa siyo rahisi kuzikamata kwa kuwa, ni mali ya shirika, japo mwenye shirika hilo ni serikali," alisema.

Shangazi alisema serikali inatakiwa kuliona hilo na kuchukua hatua za haraka ili kuepuka makandokando hayo ambayo nchi imekuwa ikiendelea kukutana nayo.

Naye, Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, alisema taifa linatakiwa kutafakari upya mifumo ya dhana ya utawala bora, kwa kuwa kuna vitendo vinafanyika waziwazi vinavyoonesha uvunjaji wa Katiba wa moja kwa moja kwa moja pamoja na kutozingatia haki za binadamu.

Alisema ipo haja ya serikali kutafakari mifumo ya kiutawala, kwa kuwa hakuna mtu mkubwa wala mdogo, mgawanyo wa madaraka upo chini, hali inayosababisha malumbano ya viongozi kila mara na kushindwa kutenda kazi ipasavyo.

"Huko marumbano ni makubwa mara Ma-DC na wakurugezi. mkurugenzi na mbunge, wakuu wa mikoa, mawaziri na makatibu wakuu vivyo hivyo mwisho wa siku mifumo inaenda ovyo.

"Suala lingine ni la uteuzi wa viongozi pamoja na ajira bila kufuata taratibu za kiushindani hali inayosababisha kupata viongozi dhaifu, watendaji dhaifu wasioweza kufanya kazi zao kwa ufanisi hali inayosababisha kumpa kazi kubwa Rais Samia Suluhu Hassan kuteua mara kwa mara," alisema.

Mpina alisema kwa sasa nafasi hizo za uteuzi zinatakiwa zishindanishwe ili kupata watu wenye ujuzi na ufanisi katika kazi, lengo ni kuondoa usumbufu kwa Rais kusoma wadhifa wa watu mara kwa mara na kudai kuwa, hata hivyo anaowachagua wamekuwa wakimkwamisha katika kazi zao.

Alimtaka waziri kuja na suluhisho la suala liloibuliwa kuhusu watu wasio watanzania kupewa vyeo pamoja na ajira nchini, akihoji kuwa ni kwa nini waziri hakuliona hilo kama changamoto katika sekta hiyo.

"Tupate majibu ya hao, waliotajwa kuajiriwa ikiwa siyo raia wa Tanzania, ni kina nani? Na kwa nini wanaendelea kuwa watumishi bila kuwa na uhalali wa kufanya kazi nchini," alihoji Mpina.

## Wachungaji wanaopinga ukeketaji wadai kutishiwa maisha, waomba ulinzi

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

BAADHI ya wachungaji kutoka kata mbalimbali wilayani Tarime, mkoani Mara wameomba Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua baadhi wa watu wanaotishia maisha yao kutokana na kupinga ukatili wa kijinsia ikiwamo ukeketaji.

Wachungaji na viongozi kutoka vyama vya siasa katika mji wa Sirari walifanya kikao cha pamoja na Jeshi hilo kujadili njia mbalimbali za kukabili uhalifu ikiwamo ukatili wa kijinsia.

Baadhi ya wajumbe walionesha kushangazwa na kuongezeka vitendo hivyo licha ya kutungwa sheria kadhaa kwa ajili ya kukomeshwa ukatili huo unaokadiriwa kufanyiwa wasichana zaidi ya 2,000 wilayani humo.

Mchungaji Julius John ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza za Kipentekoste Tanzania (CPCT), wilayani Tarime aliomba mkuu wa polisi wilaya ya kipolisi Sirari yenye kuhudumia kata zote Jimbo la Tarime vijijini, afanye uchunguzi na kuchukua hatua.

"Hivi sasa baadhi ya wachungaji kutoka kata za Pemba na Mbogi wanatishiwa maisha yao kutokana na kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile ukeketaji na wanadai kutengwa kutumia huduma za kijamii katika maeneo hayo," alidai.

Alisema zipo baadhi ya mila potofu zinazotekelezwa na baadhi ya watu wilayani humo ikiwamo kuzuia kuolewa watoto wa kike ambao hawajafanyiwa ukeketaji wakidai ni laana hali inayochangia kuongezeka vitendo hivyo.

"Lazima tushauri vijana wetu ambao hawajaingia katika ndoa kuanzia wakati huu wakubaliane kwamba wake zao wasichana ambao hawajakeketwa kama hatua kuu ya kutokomeza ukeketaji," alisema.

Mkuu wa polisi wilaya ya kipolisi Sirari, Chausiku Masasi, aliwataka wachungaji wote ambao wanadai kutishiwa wafike katika vituo vya polisi karibu yao na kuripoti watu hao wanaodaiwa kuwatishia ili uchunguzi ufanyike.

"Kila Mtanzania ana haki sawa mbele ya sheria na hakuna nafasi ya kutekeleza vitisho wala ubaguzi wa aina yoyote kwa kuwa matendo hayo ni kinyume na sheria za nchi, kila mmoja aliyeathiriwa afike haraka polisi ili hatua sahihi zichukuliwe," alisema Chausiku.

Kila baada ya miaka miwili baadhi ya jamii wilayani hapa inadaiwa kuwaondoa watoto wao wa kike shuleni ili kuwafanyia ukeketaji na wengi kati yao wanaolewa katika umri mdogo.

Mkuu wa dawati la jinsia katika Kituo cha Polisi Sirari, Neema alisema baadhi ya wasichana wanaogopa kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia kama vile ukeketaji kutokana na kuogopa vitisho vya baadhi ya walezi na wazazi.

"Tumeandaa utaratibu ambapo waathirika wote wanaofika kituoni hapo hupokewa na taarifa zao kuchukuliwa kwa siri kwa ajili ya kulinda faragha yao na kuonya walezi na wazazi wao kuwaadhibu bila sababu za msingi," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio ongezeko kikokotoo kinasubiri jibu la Rais

**KILA** inapokaribia maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, wafanyakazi wengi hutarajia serikali za nchi zao kuboresha mishahara yao ili iendane na hali halisi ya maisha.

Macho na masikio husubiri viongozi wa nchi hizo wanaposimama kwenye majukwaa kutoa ahadi au matamko mbalimbali yenye kutia moyo.

Kwa upande wa Tanzania, kilio kikubwa ambacho kila vikao vya Bunge vinapokaa bungeni ni kuhusu kikokotoo cha asilimia 33 kibadilishwe na kurudi cha asilimia 50.

Madai ya wastaafu wengi ni kuwa kikokotoo hicho hakikidhi mahitaji yao hasa ikizingatiwa kuwa walihifadhi fedha zao kwenye mifuko ya kijamii ili wanapostaafu ziweze kuwasaidia kuishi vizuri kama walivyokuwa kazini.

Katika siku ya Mei Mosi, ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi, Watanzania wengi wanasubiri kusikia lolote kuhusu kikokotoo hicho.

Juzi bungeni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, aliwaambia Wabunge kuwa suala la kanuni mpya ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu litajulikana Mei Mosi, Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Alisema hayo wakati akijibu hoja mbalimbali za wabunge na kuwahakikishia kuwa serikali haiwezi kufumbia macho wala masikio suala hilo kutokana na umuhimu wake na hasa ikizingatiwa kuwa kila mfanyakazi ni mstaafu mtarajiwa.

Hata hivyo, licha ya maelezo mbalimbali yanayotolewa ndani na nje ya Bunge, suala hilo linatarajiwa kutolewa majibu na Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi, yatakayofanyika jijini Arusha.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, Rais ameshatoa maelekezo zaidi ya mara mbili kwamba suala hiyo lifanyiwe mapitio upya kuona namna ya kukifanyia maboresho zaidi ili wastaafu wasipate shida na tayari wameanza kazi hiyo na sheria inawataka kufanyia maboresho kila baada ya miaka mitatu na tayari imepita.

Suala hilo ni maelekezo ya Rais pamoja na Bunge, lakini pengine kikubwa kinachosubiriwa ni kauli ya mwenyewe Rais katika viwanja vya Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Siku ya Mei Mosi atakapokutana na wafanyakazi kueleza suala hilo.

Pia, kwa mujibu wa Naibu waziri limepewa uzito unaostahili kuhakikisha linawekwa sawa.

Kilio cha kikokotoo kimeanza kusikika tangu serikali ya awamu ya tano, wakati kulipofanyika mabadiliko ya asilimia kwa mstaafu anayepokea kwa mkupuo mafao yake baada ya kufikisha umri wake wa kuacha kazi anapofikisha miaka 60.

Wengi wao walikatishwa tamaa baada ya kiwango cha mkupuo walichotarajia kukipata kutolingana na matarajio.

Wengi walitarajia wakipata pesa zao za mkupuo wapange mipango itakayowawezesha kuishi maisha bila kuwa tegemezi kwa wengine. Hata hivyo, kilichopatikana kiliwakatisha tamaa na wengine kupata mshtuko uliosababisha waanze kulalamika ili angalau waongezewe asilimia ya kupata kwa mkupuo.

Kilio hicho kimepokewa pia na wanaharakati mbalimbali wakiomba serikali ifikirie kuongeza kikokotoo ili wastaafu waweze kuishi maisha yenye furaha badala ya kuanza kuhangaika mitaani.

Wengine walikuwa wanamalizia nyumba zao ili waweze kuishi kwa raha, lakini walichokipata wameshindwa kufanya hivyo na matokeo yake, pesa inaishia kwenye chakula na wengine kwenye matibabu.

Kama ilivyoahidiwa bungeni, jibu linasubiriwa kutoka kwa Rais, kama kilio cha kikokotoo kitajibiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kongole wizara kuona kero mabasi ya mwendokasi

Na Sabato Kasika

**OFISI** ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imetaja vipaumbele vya bajeti yake, ikiwamo kuboresha utendaji kazi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART).

Waziri mwenye dhamana ya tawala za mikoa serikali za mitaa, Mohamed Mchengerwa, alisema hayo wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ya Sh. trilioni 10.125 kwa ajili ya wizara hiyo, bungeni jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa waziri huyo, serikali inaendelea kukamilisha Sheria ya Usafiri wa Umma ili kuihuisha DART kuwa mamlaka, hatua ambayo huenda ikaondoa kero kwenye usafiri huo.

Mabasi ya mwendo wa haraka yalianza kutoa huduma usafiri Mei mwaka 2016, lakini tangu wakati huo, usafiri wake umekuwa ukilalamikiwa na abiria kutokana na sababu mbalimbali.

Miongoni mwa sababu hizo, ni abiria kukaa vituoni muda mrefui bila kupata usafiri, kujazana ndani ya mabasi hayo kupita kiasi, jambo ambalo linaonekana hakuna unafuu wa usafiri waliotarajia kuupata.

Kero hizo na nyingine nyingi, zimekuwa zikisababisha baadhi ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam kuomba serikali kurejesha usafiri wa daladala katika ruti zinazotumiwa na mabasi hayo.

Kwa mfano; ruti ya kutoka Mbezi Mwisho hado katikati ya jiji, hakuna daladala, badala yake yanatumika mabasi hayo tu, ambayo kimsingi hayawezi kumudu wingi wa abiria walioko Mbezi.

Abiria wanaoamka alfajiri kuwahi shughuli zao katikati ya jiji, wamekuwa wakitumia usafiri wa daladala zinazoiba ruti kabla askari wa usalama barabarani hawaingia kazini.

Bila usafiri huo wa daladala zinazoiba ruti, wengi wangekuwa wanakwama kuwahi katika shughuli zao, kwa sababu mabasi ya mwendo wa haraka hufika kituo cha Mbezi Mwisho kuanzia saa 11 alfajiri.

Katika mazingira hayo, wamekuwa wakiomba usafiri wa daladala urejeshwe kwenye Barabara ya Morogoro kuanzia Mbezi Mwisho hadi katikati ya jiji badala ya kutegemea mabasi hayo tu.

Mbali na ombi hilo, pia wamekuwa wakitamani kuwapo viongozi wa wakala wa mabasi hayo wanaofuatilia mwenendo wa usafiri kila siku ili eneo ambalo lina abiria wengi, mabasi yapelekwe eneo hilo.

Wanatolea mfano usafiri wa zamani wa UDA, kwamba kulikuwa na viongozi ambao walikuwa wakizunguka maeneo mbalimbali ya jiji kuona hali ya usafiri ili kuongeza mabasi penye abiria wengi.

Kama nilivyoeleza, Mbezi Mwisho ni miongoni mwa maeneo yenye kero kwa usafiri wa mabasi hayo, abiria wanalazimika kujipanga mistari miwili, ikiwamo wa wale wanaokaa kwenye viti na wanaosimama.

Hiyo yote inatokana na uhaba wa mabasi hayo, hivyo, abiria wanalazimika kukubali kubanana ndani ya mabasi hayo kwa sababu hakuna usafiri mwingine, ili wawahi katika shughuli zao za kila siku.

Matarajio ya wengi yalikuwa ni kuona kero za usafiri jijini Dar es Salaam, zilizokuwa zinasababisha na daladala ikiwamo kukatisha ruti na kupandisha nauli kiholela, zinaisha.

Lakini badala hata ya kuja mabasi hayo, kero zimeendelea kuwapo kana kwamba ni jambo la kawaida abiria kukosa usafiri au kujazana ndani ya vyombo hivyo vya usafiri.

Kwa kuwa wizara imeamua kuboresha utendaji kazi Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), ninadhani kero zote, ambazo abiria wamekuwa wakikutana nazo katika usafiri huo, zitapatiwa ufumbuzi.

Hatua zinazochukuliwa na serikali za kutaka kuboresha utendaji wa DART, zisaidie kuufanya usafiri huo usiwe kiraha bali uwe raha kama ambavyo watumiaji wake walitarajia.

Kwa maana hiyo, wizara iangalie kero hizo zinazolalamikiwa, kwani itakuwa haina haja kupanua usafiri huo maeneo mengine ya jijini kama ambavyo barabar za mabasi hayo zinaendelea kujengwa.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA

# Kama uamuzi wa mahakama wa haki, kwa nini serikali na Bunge, hazijautekeleza?



Pascal Mayalla

LEO naendelea na zile makala zangu elimishi kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) kwa jicho la mtunga katiba, alidhamiria nini wakati anaweka kifungu fulani ndani ya katiba yetu.

Leo pia nashauri tu kwa mihimili yote mitatu, ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama japo yote wajibu wa kuheshimiana, kutoingiliana, katika kuilinda na kuitetea Katiba ya JMT, inapaswa kudhibitiana na ikibidi kuadhibiana kama kuna mmoja wapo unavunja katiba hii.

Huko nyuma, niliwahi kumzungumzia Mchungaji Christopher Mtikila (Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi) alivyofungua kesi ya kikatiba kupinga sharti la mgombea uongozi kudhaminiwa na chama cha siasa, akapewa ushindi kwa Mahakama Kuu kutamka kifungu hicho ni batili.

Mchungaji Mtikila, mwaka 1993, alifungua kesi Na. 5 ya 1993 akifanya juhudi kubwa kukipinga kifungu hiki na Mahakama Kuu kupitia kwa Jaji Kahwa Lugakingira (Mungu amuweke mahala pema peponi), ikatamka wazi na bayana kipengele hicho ni batili na kinakiuka katiba ya JMT ya mwaka 1977, hivyo kifutwe na kutoa haki kwa kuwa kila Mtanzania ana haki ya kushiriki kugombea uongozi.

Serikali ilikata rufani na wakati huo huo ilipeleka Bungeni kwa hati ya dharura, sheria Na. 34 ya mwaka 1994, kufanya marekebisho ya nane ya Katiba ya JMT na kukichomeka kipengele hicho batili cha mgombea kudhaminiwa na chama cha siasa, ndani ya katiba, hivyo kuibatilisha ile hukumu ya Jaji Lugakingira! Hapa ndipo ubatili wa kuinajisi katiba yetu ulipoanzia kwa serikali yetu kuchomekea ubatili ndani ya katiba yetu kiubatili.

Mchungaji Mtikila, licha ya kuwa ni mwanasiasa, mwenyekiti wa chama cha siasa cha DP (Democratic Party), alikuwa ni mtu wa Mungu kiukweli kabisa, kwa sababu hakukubali kabisa katiba yetu ichezewe, hivyo akafungua kesi nyingine No. 10 ya mwaka 2009 kupinga marekebisho hayo ya nane ya Katiba na kuyaita ni ubatili!.

Katika kesi hiyo, Mchungaji Mtikila aliomba mambo mawili makuu, kwanza, Mahakama Kuu itamke ibara 39 na 67 za Katiba zilizorekebishwa na marekebisho hayo ya na kwa sheria Na. 34 ya mwaka 1994 ni batili na kinyume cha katiba.

Pili, aliomba Mahakama Kuu kutamka wazi kuwa Kila Mtanzania ana haki ya kugombea kwa mujibu wa ibara ya 21 ya Katiba, bila kulazimishwa kudhaminiwa na chama cha siasa, hivyo mtu anaweza kugombea kama mgombea binafsi.

Mahakama Kuu chini ya majaji watatu, (majaji watatu kisheria inaitwa half bench), Amiri Manento, Salim Masati na Thomas Mihayo, wakayakubali mambo yote ya Mchungaji Mtikila na kumpa ushindi tena kwa kutamka marekebisho hayo ya 8 ya katiba ya JMT, ni batili!, Ibara za 39 na 67 ni batili zifutwe toka kwenye vitabu vya sheria.

Lakini serikali yetu, ikakata tena rufani na safari hii Mahakama Rufaa ikakaa chini ya majaji saba akiwamo Jaji mkuu Augustino Ramadhani, akisaidiwa na majaji Eusebia Munuo, January Msoffe, Natalia Kimaro, Salum Mbarouk, Bernard Luanda na Mjasir na Juni 17 2010 ikatoa uamuzi wa ajabu kabisa kuwahi kutokea Tanzania! Tena Mahakama haikuwa peke yake, bali iliwaita mabingwa wabobezi wa sheria na katiba kuisaidia, kwa lugha ya kimahakama ni marafiki wa mahakama (Amicus Curiae) ambao ni Othman Masoud Othman, Prof. Palamagamba Kabudi na Prof. Jwan Mwaikusa (Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi).

Uamuzi wa Mahakama ya Rufani ulifanya kituko katika kutii ukuu wa katiba. Kwa ajili ya kulinda heshima ya mhimili wa Mahakama, na mimi kwa vile ni wakili, hivyo ni pia ni ofisa wa mahakama, ili nisije kuonekana mtovu wa nidhamu, kwa kuivunjia heshima Mahakama, naomba kukuwekea sehemu ndogo tu ya hukumu yenyewe.

"So as to let the will of the people prevail as to whether or not such [independent] candidates are suitable. We are definite that the Courts are not the custodian of the will of the people. That is the property of elected Members of Parliament"

Tafsiri ni kwamba: "Ili kuruhusu matakwa ya watu kutawala kama wagombea hao [huru] wanafaa au la. Tuna uhakika kwamba Mahakama si wasimamizi wa matakwa ya watu.

Hiyo ni mali ya wabunge wa kuchaguliwa".

Hapa Mahakama ya Rufani, haikuwatendea haki kabisa Watanzania.

Katiba ndiyo matakwa ya wananchi (the will of the people). Katiba imekukwa serikali kupeleka bungeni muswada wenye kipengele batili kinachokwenda kinyume cha katiba ya JMT na Bunge likaitunga sheria hiyo batili, Rais akatia saini kuidhinisha ianze kutumika.

Mahakama kuu ikaibatilisha kuwa ni batili!, serikali ikapeleka bungeni mabadiliko ya katiba kwa hati ya dharura kuuchomekea ubatili ule ndani ya katiba yetu, Bunge likauchomeka!

Mahakama Kuu ikatoa hukumu ya pili kuwa huo ni ubatili na mabadiliko hayo ni batili, Mahakama ya Rufani ikaurudisha ubatili huo kwa mhimili wa Bunge kuuondoa! Huku si kuwatendea haki Watanzania?

Swali kubwa zaidi la kujiuliza ni kwa nini mpaka leo, serikali na bunge, hazijauondoa ubatili huo ndani ya katiba yetu?!

**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wapinzani mbona hamjaanza kama wenzenu?



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

UKIKAA na redio au luninga yako ukisikiliza na kutazama hasa kipindi cha Bunge, hutaamini kwamba nchi hii ina matatizo hususan ya kimaisha kwa baadhi ya watu wake hasa wa kipato cha chini.

Na ukitafakari kwa kina na kufuatilia mijadala, utashindwa kubaini tofauti baina ya Mbunge na Waziri, lakini hutaona kabisa mgawanyo kati ya chama tawala na upinzani katika Bunge la sasa.

Kwa hili la mwisho la pande mbili za Bunge ni dhahiri, kwani kilichojiri enzi za Rais John Magufuli hasa baada ya uchaguzi mkuu mwaka 2020, kinaonesha sababu ya kuwapo kwa hali hiyo.

Ni mwaka ambao upinzani ulikaribia kuambulia patupu katika uchaguzi wa wabunge, na mbaya zaidi ni pale kulipotokea la kutokea kwa kuibuka wabunge wa viti maalumu kutoka upinzani waliobatizwa jina la UVIKO-19.

Hivi sasa ni sawa na kusema tu, kuwa ni Bunge la chama kimoja ingawa si rasmi, lakini mwenendo uko hivyo, na ndiyo sababu mwanzo mwisho ni sifa kwa Dokta Samia Suluhu Hassan kwa kutoa mabilioni ya pesa za miradi.

Mwanzo mwisho, mbunge na waziri wanasimama wanatamka wakihamasisha kwa kaulimbiu ya 'Simama na Samia', na kuhanikiza kuwa mwaka 2025 ni nani kama si Samia.

Unamsikiliza mbunge, badala ya kusema ya waliomchagua kwa maana ya kero na matatizo yaliyoko jimboni, anazungumzia mafanikio ya Serikali katika jimbo, anachukua nafasi ya Serikali anageuka kuwa Waziri.

Kwa kawaida kama ambavyo tulizoea katika mabunge yaliyopita hata yaliyokuwa chini ya chama kimoja cha TANU na hatimaye CCM, wabunge walijitofautisha na mawaziri.

Wabunge walikuwapo ili kuuliza maswali na kutaka majibu na ufafanuzi kulingana na walivyotumwa na wapiga kura wao, huku mawaziri wakijibu, wakifafanua na kutoa mwelekeo wa nini kifanyike.

Inashangaza leo, tena katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, wabunge wa CCM wanasimama na mawaziri wao ambapo haikwepeki ni wa CCM pia, kusifia kilichotekelezwa na Serikali na kusahau kuwa ni wajibu wake.

Baba au mama akileta chakula nyumbani, akimnunulia mwanawe mavazi, akimsomesha mwanawe ni wajibu wake wa msingi na si asifiwe kiasi hicho, bali ashukuriwe tu kwa alichokifanya na si kwa kupindukia.

Leo Serikali inatimiza wajibu wake, inasifiwa kana kwamba inajitolea kufanya hivyo, na kujisahaulisha kuwa wananchi ndio waajiri wake na wanapolipa kodi wanastahili kulipwa kwa maendeleo.

Naamini hizo sifa anazopewa Rais Samia hata yeye hazifurahii na hasa zile zinazojichanganya na uchawa ambao pia naamini haupendi, lakini anashindwa kuukana hadharani kutokana na muktadha wa kisiasa uliopo, inabidi kuvumilia tu.

Kimsingi, kwa wanaomjua Rais Samia si mtu mpenda madaraka na kusifiwa, si mtu anayejivuna, bali mwenye roho isiyopenda kuumizwa lakini pia yenye huruma kwa mtu mwingine anayetaabika.

Pengine ndiyo sababu hujikuta akiambiwa mambo mengine, yakiwamo ya kutungwa na kuyanyamazia tu, kwa sababu anaona akizusha mabishano sisi tutashindwa kumtofautisha na anayempa uzushi.

Wanaomsifia kwa kumpaka mafuta kwa mgongo wa chupa, wanataka kujishajihisha kwake ili waonekane wako naye, lakini kumbe wanataka kumtumbukiza korongoni kisiasa bila kujitambua.

Mbaya zaidi, sasa tunashuhudia kampeni zinzoanza kinyemela kwa sifa lukuki kila mahali na kaulimbiu tata kila siku, ilimradi watu kujionesha kwake, wako tayari kumpigia kura mwakani lakini ikumbuke, kura ni siri.

Kila kukicha zinachangwa fedha za kumchukulia fomu ya ugombea pekee ndani ya CCM na hao hao ambao leo tunaambiwa ndio wanaofadhili watu ili wamtukane mitandaoni, huku wakidai wanasimama na Samia!

Ni bahati mbaya sana, sijasikia bungeni katika Bunge hili la vyama vingi vya siasa, akisimama mpinzani na kusema anasimama pengine na Freeman Mbowe, Tundu Lissu, Zitto Kabwe au Hashim Rungwe! Ina maana wao hawagombei mwakani?

Yawezekana wapinzani wanaheshimu kanuni na taratibu zilizopo, kwamba kwa kuwa uchaguzi bado hivyo si wakati wa kampeni, au pengine hawana watu wa kusimama dhidi ya Samia kwenye kinyang'anyiro?

Kama wapinzani mnadhani hamna watu wa kupeperusha bendera zenu kwenye uchaguzi ujao, basi semeni ili tuokoe fedha za kugharimia uchaguzi ili Rais Samia apite bila kupingwa na aendelee na urais mpaka mwaka 2030! Wenzenu wameanza ninyi je?

Ni vema wapinzani nao wakaanza kunadi watu wao, ili nasi wapoiga kura tuanze kufanya tathmini na kujua nani atatufaa mwakani bikla kujali chama, kwani masuala ya kuchagua vyama yamepitwa na wakati sasa tunataka watu wenye uwezo na weledi.

Tukiwasililiza Makamu Mwenyekiti wa CCM, Bara, Abdulrahman Kinana na atibu Mkuu wa Chama hicho, Dk Emmanuel Nchimbi kughusu uchaguzi bila shaka tutaona tunakoelekea! Wasibadilike tu mwishoni. Siasa za Bongo zinajulikana!

# Mafunzo uanagenzi kutolewa Chuo cha CBE

**Na Restuta James**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kinakusudia kuanzisha mafunzo ya uanagenzi kwa wanafunzi wanaosoma shahada ya masuala ya benki na fedha na metrolojia na viwango, ambayo itawawezesha kusoma huku wakifanyakazi.

Akizungumza katika Siku ya CBE Atamizi (Incubation Day), jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa chuo hicho, Profesa Edda Lwoga, alisema lengo ni kuwawezesha wanafunzi kuhitimu masomo wakiwa na ujuzi unaohitajika katika soko la ushindani wa ajira.

Alisema katika utaratibu huo, mwanafunzi atasoma muhula mmoja chuoni na muhula mwingine kwa mwajiri, ambako utakuwa anapata mafunzo kwa vitendo.

"Kwa hiyo mwanafunzi atasoma mwaka mmoja na nusu chuoni na mwaka mmoja na nusu kwa mwajiri. Tumeshaingia makubaliano na baadhi ya taasisi ambazo ziko tayari kuwapokea wanafunzi kwa mafunzo ya vitendo," alisema.

Kuhusu uatamizi, Profesa Lwoga, alisema lengo la programu hiyo ni kuwawezesha wanafunzi kuwa wabunifu na kutumia elimu ya darasani kutengeneza biashara halisi.

Alisema wanapatiwa mafunzo sahihi kuhusu mawazo yao ya biashara, mitaji na kuwaunganisha na wafanyabiashara pamoja na taasisi zinazohusika na ubunifu wao.

Alisema tayari wanafunzi 282 wanaatamiwa ambao wameanza kutengeneza bidhaa na mifumo ya kutatua changamoto mbalimbali kwa jamii.

Akizungumza katika tukio hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa benki ya Finca, Edward Talawa, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema moja ya nyenzo muhimu ambayo wabunifu wanapaswa kuwa nayo ni nidhamu ya fedha na kwamba, benki yake itatoa nafasi ya uanagenzi kwa wanafunzi wa CBE.

Alisema ubunifu uliofanywa na CBE utasaidia kutatua changamoto ya ajira nchini, kwa kuwa itazalisha wajasiriamali ambao watajiajiri na kuajiri wengine.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Ushirika wa wajasiriamali wahitimu wa Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA), Revocatus Kimario, alisema wanafunzi wana nafasi ya kupata masomo ya vitendo katika nchi za Ulaya na kuwataka walio katika programu ya uatamizi kuzichangamkia.

Baadhi ya wanafunzi waliopo kwenye programu ya uatamizi, alisema wanakabiliwa na ukosefu wa mitaji na masoko ya uhakika wa bidhaa na huduma zao.

# Nchimbi: Changamkieni mikopo 10%, puuzeni maandamano

**Na Halfani Chusi**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimewataka wananchi kupuuza maandamano yanayoandaliwa na Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), badala yake watumie muda wao kwenda kuchukua mikopo ya asilimia 10 iliyorejeshwa na serikali.

Katibu Mkuu CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alitoa kauli hiyo juzi wakati akihutubia wananchi mkoani Njombe na kuonya baadhi ya viongozi wa CCM kuwa madalali kwa wanaotaka kuwa viongozi na kusisitiza tabia hiyo itafarakanisha chama.

Alisema kazi kubwa iliyofanywa na serikali ndani ya miaka mitatu ni nyenzo inayobeba ukweli wa kutosha kusambaratisha uongo unaoenezwa na baadhi ya wapinzani wa kisiasa kupitia mikusanyiko yao.

Balozi Nchimbi aliwataka wanaCCM wote kuendelea kujiamini na kutembea kifua mbele wanapozisema, kuzitangaza na kuikumbusha jamii kuhusu kazi za maendeleo na ustawi wa jamii, zinazofanywa na serikali ili wananchi waendelee kuona ukweli, wakitofautisha na uongo unaoenezwa kwa propaganda nyepesi za kisiasa.

"Mambo yaliyofanywa na serikali ndani ya miaka mitatu, unaweza kuona kama ni miujiza, kazi kubwa sana inafanyika ni wajibu wetu kuyatumia mazuri hayo kukipambania chama," aliagiza.

Aliwasisitiza watendaji wa chama na serikali ulazima na umuhimu wa kuwa waadilifu wakati wote kwenye masuala yanayohusu rasilimali za umma, kwa kupiga vita rushwa na ubadhirifu.

Pia, aliwataka wananchi kulinda miradi inayotekelezwa na serikali akiwataka kuitunza kwa wivu mkubwa na uzalendo.

"Serikali ya CCM inatekeleza miradi mingi na inatumia fedha nyingi za umma, lazima viongozi wahakikishe fedha zile hazipotei zinatumika kulingana na maelekezo ya serikali.

"Viongozi wa dini na wa kimila endeleeni kusisitiza uadilifu ndani ya nyumba na nje ya nyumba zetu ili tujenge chama imara, lazima wana-CCM tuwe na umoja. Simamieni haki bila kubaguana kwa itikadi za siasa, dini, na ukabila.

"Tufanye kazi ya kutangaza mazuri ya CCM, kwa miaka mitatu kazi iliyofanyika Njombe ni kama miujiza. Kuna wakati watu wanasahau mazuri yaliyofanywa na serikali. Kuna watu watazunguka huko watasema, chama hakijafanya lolote, mtu wa aina hiyo mpuuzeni, lakini mpingeni kwa hoja."

Kupitia mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, aliwasilisha taarifa ya mrejesho wa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2020-2025, iliyohusisha miradi mbalimbali ya maendeleo na ustawi wa wananchi.

Katika ziara yake, Balozi Nchimbi wakati akielekea Songea, alipitia Wilaya ya Madaba, mkoani Ruvuma na kusalimia wananchi wa eneo hilo na kuwaahidi serikali itaendelea kununua mazao kwa wakulima ili kuwaepusha na wafanyabiashara wanyonyaji.

Katika ziara hiyo, Nchimbi ameambatana na Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amosi Makalla na Katibu wa Oganaizesheni, Issa Gavu.



Wananchi wakichagua nguo katika Mtaa wa Kongo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# PM azindua studio kidijitali TBC

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua studio za kidijiti za redio ikiwa ni sehemu ya mradi wa maboresho ya studio za redio, televisheni na mitandao ya kijamii za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Katika uzinduzi huo, Majaliwa alifanyiwa mahojiano na kufunguka namna alivyofanikiwa kupata kazi ya utangazaji mwaka 1994 na kabla kuripoti kazini, akachaguliwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Majaliwa aliyasema hayo jana katika uzinduzi huo uliofanyika katika studio za shirika hilo zilizoko barabara ya Nyerere, jijini Dar es Salaam.

"Nimefurahi sana baada ya kujulishwa kuwa uzinduzi wa mradi huu umezingatia awamu ya tatu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026). "Mpango huo umeainisha vipaumbele katika uwekezaji wa miundombinu ya utangazaji ya TBC, ikiwemo upanuzi wa usikivu wa redio, ununuzi wa mitambo na vifaa vya redio na televisheni," alisema.

Katika mahojiano hayo, Majaliwa alisema alifanikiwa kupata kazi hiyo, lakini kabla hajaripoti akawa amechaguliwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Nilitakiwa kuanza kazi Julai 10, 1994, lakini matokeo ya kwenda Chuo Kikuu yakatoka mwezi Juni. Wazee wakanishauri nikasome kwanza, nikimaliza nitakuja kuomba kazi, lakini baada ya chuo, nikaishia huko," alisema. Pia, alitembelea studio za TBC International na Bongo FM ambako alikuta vijana ndiyo wanashika usukani wa kuendesha mitambo na vipindi na kuelezwa na Mkurugenzi wa Huduma za Redio, Aisha Dachi, kwamba maudhui yake yamewalenga zaidi vijana.

Waziri ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema mafanikio hayo yote yanatokana na utashi wa kisiasa wa Rais Samia Suluhu Hassan, wa kuamua kuwekeza katika shirika hilo.

Waziri Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa SMZ, Tabia Maulid Mwita, alimshukuru Waziri wa Habari, Nape kwa kuwasaidia Tume ya Utangazaji Zanzibar kupitia TCRA kwa kuwapatia vifaa vya sh. milioni 45.

Mkurugenzi Mkuu wa TBC, Dk. Ayub Rioba, alimweleza Waziri Mkuu kwamba, shirika hilo hivi sasa ni miongoni mwa vyombo vya habari vya kupigiwa mfano barani Afrika.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Suleiman Kakoso, aliitaka Wizara ya Habari kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ziitumie TBC kuandaa vipindi vipya ambavyo vitatumika kuitangaza nchi.

# MAISHA

APRILI 21, 2024
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



## HARUSI

Ukurasa 12



**FURAHIA MAISHA**
**Ukitembea kwenye mvua**

Ukurasa 13



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Fahamu sababu zinazochangia nyumba kuvuja muda mfupi baada ya kujengwa



**SUPU YA KAROTI**

Ukurasa 14





## ONDOA UKAVU kipindi cha baridi

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| N | ■ | D | I | M | B | A |
| I | ■ | ■ | ■ | W | ■ | N |
| P | ■ | G | O | A | ■ | G |
| A | N | A | ■ | G | I | A |
| S | ■ | N | O | A | ■ | L |
| H | ■ | Z | ■ | ■ | ■ | I |
| E | L | I | M | U | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MBA, BEE, ZII, LAO, IFATE, SKETI, BOMBA, ELEZA, IMBISHA, SHULENI

## TOA TOFAUTI 5





## AMSHA AKILI

HAYA WATOTO WAZURI, KATIKA MCHORO HUU, KUNA BATA WANNE NA SAMAKI WATATU WAMEJIFICHA. HEBU TUONESHE KWA KUWAWEKEA VIVULI.



## PAKA RANGI




**Alichokifanya daktari**

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanangu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Ushuhuda mchawi alivyokuwa anawapeleka watu kuzimu

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na ushuhuda wa mchawi mmoja aliyeamua kujilipua hadharani na kutoa siri zote. Baadaye akaokoka kwenye kongamano la dini lililoongozwa na Mchungaji Ezekiel kutoka Kenya kwenye uwanja wa Biafra, Kinondoni Dar es Salaam, Machi 22, mwaka huu.

Hii ni sehemu ya tatu ya simulizi hii. Mtu huyo alielezea jinsi alivyoshirikishwa katika uchawi ambao alisema pia ukoo wao ulikuwa ni wachawi wakubwa. Akataja baadhi ya silaha wanazotumia kufanya ushetani huo kuwa ni pamoja na Simba, chatu, nyuki, vyura na fisi.

Akaelezea mambo ya kichawi aliyofanya katika maisha yake hadi kupelekea kukatwa mguu baada ya kukiuka masharti kwa wakuu wake wa kichawi. Baada ya ulemavu huo akakimbilia kuokoka. Sasa endelea anavyoeleza mwenyewe.

Akasema alioa wanawake 16. Kwa sana ana moja tu yule wa mwisho. Ana watoto wa kike wanne warembo sana. Lakini hakuna mwanamume aliyekosea hata namba aje awaoe. "Niliua sana sana mimi. Yaani mahakimu nimeua sana hata askari. Nikimpa saa tano hayupo duniani.

> **"Tunawachukuwa usiku kwenda kuwalimisha na kuwafanya viti vya kukalia, tunaenda kuwalisha nyama.**

Tuseme askari anyoshe kidole anipige kofi, siku hiyo atapigwa sana usiku kucha na anakufa kwa kipigo. Mchungaji Ezekiel akamwuliza ni nani atampiga akajibu: "Nilikuwa na maskadi yangu nilikuwa nayaagiza".

Kama kuna mtu amedhulumiwa hela na kuniambia nimuadhibu aliyedhulumu, mimi huenda kusimama barabarani namwaga dawa, gari lilolopanda aliyedhulumu likipita linapata ajali na anakufa tu yule aliyedhulumu.

Ezekiel: Kwa hiyo ajali hizi haziwezi kuzuilika kwa kutengeneza barabara safi?

Mchawi: Haiwezekani.

Ezekiel: Na kuwa watu wanakufa lakini hawakustahili kufa kabisa?

Mchawi: Labda awe ni Mlokole. Lakini huu ulokole wa kumsifu tu Bwana.

Ezekiel: Kwa hiyo unatuambia katika ulokole wapo na viwango vya nguvu?

Mchawi: Kuna mlokole mwingine ukimjaribu unajisikia kuwa moto na hauthubutu. Lakini wengi, asilimia 68 ni walokole feki, tunawabeba kwenda kuwafanya ni viti vyetu vya kukalia sisi wafalme.

Tunawachukuwa usiku kwenda kuwalimisha na kuwafanya viti vya kukalia, tunaenda kuwalisha nyama.

Ezekiel: Wakishakula nyama inakuwaje?

Mchawi: Yeye akisha kula hizo nyama tu tayari anaingizwa kwenye chama.

Ezekiel: Viwango vya kuzimu havilingani.

Mchawi: "Mchungaji, Gambushi ni eneo ambalo huwezi kuliona kwa macho ya mwili na nyama. Lakini katika ulimwengu wa roho kwa sisi ambao ni wachawi ni eneo kubwa kabisa kama ulivyo mkoa wa Dar es Salaam.

Huko yapo magari, mapikipiki, kuna wainjilisti, waimbaji maarufu ambao wanamwimbia Mungu lakini hawana Mungu. Humo kuna kwaya za kila aina.

Ezekiel: Wanalala usiku kwao, kumbe wanaimba huko gambushi.

Mchawi: Mtu anakufa, wanazika mgomba sisi tunamchukua tunapeleka. Mnazika mbwa, sisi tunapeleka mtu anayedaiwa kufa.

Ezekiel: watu wanaona wamezika mtu kumbe ni mbwa?

Mchawi: Ndio, sisi tumeshabeba

Ezekiel: Huyo mtu anaenda kuwa mwimbaji kule?

Mchawi: Mtumwa hadi kufa kwake. Inajulikana amekufa kumbe hajafa. Sisi tunampeleka huko atazeeka na atakufa. Lakini hatukubali afe tumzike, kama amebakiza muda kidogo afe, tunamchinja, tunamtoa mafuta kwa ajili ya mambo mengine.

Ezekiel: Hayo mafuta yanafanya nini?

Mchawi: Tunayatumia mfano watu wanakula nyama kwenye sherehe, nachukua hizo nyama na kuwawekea hayo mafuta wanakuwa wanakula vitu vingine.

Wao wanadhani wanakula nyama kumbe nyama ya mbwa, ya fisi, sisi tunabeba nyama tunapeleka kwenda kula. Au watu wanaweza kuwa wanakunywa soda, basi naweza kubadilisha hiyo soda nikaweka soda ya mkojo.

Kufikia hapo, Mchungaji Ezekiel akasema, sisi watu wateule tuliopewa nguvu za Mungu tunapaswa tuwe na maisha mazuri, tujenge nyumba, wengine waolewe na kadhalika, wachawi tunataka wafe!

Bila shaka msomaji wangu umepata picha jinsi mambo yanavyofanyika katika ulimwengu wa giza unaotawaliwa na shetani. Wapo watu wanaojikuta wakifanya mambo mabaya pasipo wao kutaka kama baba huyu.

Hakupenda mambo ya kichawi lakini akalazimishwa. Na hata alipojaribu kukataa alikumbana na adhabu kali kama alivyopigwa na nyoka na pia kukatwa mguu.

Wako watu waliowatoa kafara wanafamilia, baba, mama, watoto kwa udanganyifu wa shetani ili kupata na mali nyingi. Hata hivyo, watu wa aina hii wameishia pabaya sana. Kazi ya ibilisi ni kuharibu, kuchinja na kuua.

Tafuta nguvu ya Mungu mpendwa uwe salama.

***Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Ni ngumu kuwa na kanuni moja ya kufikia ndoto zetu

AIBU yako ndio mtego wako. Fursa nyingi katika maisha zimefichwa kwenye mambo ambayo tunaona aibu kujihusisha nayo au kuyafanya.

Walimwengu wanasema wakati ukifika huwa hauna makengeza na aliyekusudiwa kwa wakati ule atakuwa tu na asiyekusudiwa kwa wakati husika hatakuwa.

Kama ndivyo basi ni muhimu tuheshimu nyakati za watu, ili na wewe ujenge nafasi ya kuheshimiwa wakati wa nyakati zako.

Unanisikia au niongeze sauti! Ni hivi! Usihusudu, wala kuingiwa na tamaa na nyakati za watu. Jenga tabia ya kuheshimu nyakati za watu kwa sababu nyakati huzunguka.

Pale mahali hazina yako ilipo, ndipo moyo wako ulipo. Kuna uhusiano mkubwa kati ya haya nayoyasema na uhusiano wako na Mungu. Sasa sijui umeyaweka wapi?

Mosi, wako wanaodiriki kusema kama maisha ninayo, watoto ninao na mali ninazo, hivi nahitaji nini kingine? Wanasahau kuna nyakati, wanasahau kuna Mungu aliyewatoa sehemu moja kwenda nyingine.

Hawakumbuki ni yeye aliyewavusha. Acha kiburi kaka, acha kiburi dada! Ni wangapi waliotafuta mali na kujilimbikizia utajiri wa kufuru na leo wameshushwa vyeo, walikutana na kile kinachoitwa uteuzi na utenguzi?

Ubaya huwa haujifichi. Yaani huna tofauti na wale ndugu wanagombania, wanatesa watoto au familia ya mwenzie.

Unadiriki kusema hadharani tena kwa majigambo, haiishi mpaka iishe. Unakimbilia kupeleka kesi mahakamani ili nini? Vitu vya ulimwengu huu visikugombanishe.

Mara umenunua kiwanja unapost (unachapisha mtandaoni), unaanza kujenga una-post. Mwisho wa siku ujenzi unakwama!

Ndugu yangu, wakati mwingine hufanikiwi kwa sababu unatangaza ndoto zako kabla hazijawa! Usisahau sio kila mtu anafurahia mafanikio yako.

Labda hujanielewa. Hizo ndoto zako za kutaka ukubwa, cheo na umaarufu hakuna tatizo. Ni mfululizo wa picha, mawazo, mihemko na hisia ambazo hutokea akilini, kwa kawaida bila makusudi.

Mambo yote hayo huja katika hatua fulani fulani za usingizi; na wakati mwingine zikawa ni ndoto za mchana kweupe.

Usitangaze ndoto yako, tangaza matokeo, vinginevyo utaishia kuuzwa utumwani kama Yusufu. Yusuph akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia.

Pia, historia isikuzuie kutimiza ndoto yako. Ni muhimu kuwa na utamaduni wa kuheshimu ndoto zetu, hata kama tunadhani kuwa ni ndoto ndogo kama vile ndoto ya kumiliki aina fulani ya mali. Wengi husema wanataka kutimiza ndoto zao, hata hivyo ni wachache hufanikiwa kutimiza ndoto zao.

Kwa kuwa binadamu tuna ndoto tofauti tofauti. Ni ngumu kuwa na kanuni moja ya jinsi ya kufikia ndoto zetu, hata hivyo uzoefu unaonyesha mambo kadhaa ambayo watu wengi walifikia ndoto zao wamefanya.

Kuota ndoto ya mabadiliko ya maisha yako, sio tuu kuwaza au kutamani kufikia hali fulani, bali kuota kwa usahihi ni kutengeneza picha kichwani ya hali unayotaka kufikia, au mambo unayotaka kuyapata.

Mungu hawezi kukuacha ukafa bila kutimiza ndoto zako utaona unapita kwenye misukosuko mingi lakini bado unaishi. Wakati mwingine Mungu hutuma malaika waje wakusaidie bila wewe kujua.

Ni kama ule wakati wa Ibrahimu alikwua katika shida na mkewe Sarah alikuwa hana mtoto, malaika wakaja kwake wakamwambia Sarah atapata mtoto ni kama kipindi cha Sodoma na Gomora, malaika wakaja wakamwokoa Lutu na familia yake.

Iko hivi malaika akija katika ulimwengu wa mwili, yaani duniani anavaa mwili kama ulionao wewe; ndio maana kuna watu mmesaidiwa na watu msiowajua hata mkiwatafuta muwashukuru.

Hamtawaona tena hao walikuwa malaika na anaweza akaja akavaa mwili wa kidhaifu kabisa wala usimjue.

Wabaya wako ndio watakuwa viongozi wa kupiga makofi kwenye mafanikio yako. Halafu iko siku moja, wabaya wako watafitinishana katika hila zao.

Cha ajabu ni kwamba inaweza ikatokea wewe ndio ukawa msuluhishi wao.Sijui naeleweka! nasema hivi wachekee wabaya wako ili wasijue kama unajua ubaya wanaokufanyia.

Wengine waache walalamike. Hawalalamiki ili wasaidiwe namna ya kuishi. Wanalalamika angalau wasinyang'anywe haki yao.

*Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com na Simu ya mkononi +255 715 545 490*

# HARUSI








Ni kumbukumbu iliyotukuka kati ya Mercy George Ndoyela 'Papaa' na Christina Lalay wakati walipofunga ndoa katika Kanisa la Mtakatifu Columbus Pugu, jijini Dar es Salaam na kufuatia sherehe fupi katika ukumbi wa Kinondoni Vijana Social .

Na Moshi Lusonzo





# FURAHIA MAISHA

## Ukitembea kwenye mvua

MVUA za masika zinaendelea kunyesha, lakini shughuli za kimaisha nazo zinasonga mbele bila kukoma.

Katika kipindi hiki, koti la kuzuia mvua ni suala la msingi katika kuhakikisha hukwamishwi na hali ya hewa katika harakati zako za kimaendeleo.

Kimsingi aina hii ya vazi hutengenezwa kwa lengo la kujilinda dhidi ya maji ya mvua na lina uwezo kukupa joto sahihi.

Watengenezaji hutumia suluhisho tofauti na wakati mwingine teknolojia tofauti za kisasa. Hata hivyo kiwango cha kuzuia kupenya maji daima huwa sawa.

**JINSI YA KUCHAGUA**

Kitu cha kwanza katika kuchagua koti la mvua, angalia ukubwa wake. Lakini hapa kila mtu ana chaguo lake na hakuna kanuni ya uvaaji kutokana na ukubwa wa koti.

Kuna baadhi ya watu wanapendelea kuvaa makoti marefu, wengine mafupi na wengine yaliyobana. Wote wapo sawa ili mradi hawaathiriki na mvua.

Ikiwa unataka kuhifadhi vitu visiliwe, chukua koti lenye mifuko ya juu yenye mifuniko imara. Mifuko ya juu huiruhusu maji kulifikia ukiwa umevaa vazi lako.

Pia chagua koti lenye uwezo wa kuhifadhi joto sahihi ili kukuhakikishia furaha wakati wote.

## UREMBO

Na Mary Geofrey





MSIMU wa mvua nyingi unaendelea huku tukitarajia kuingia katika kipindi cha baridi ambacho idadi kubwa ya watu watakumbwa na athari ya kukauka kwa ngozi.

Watu wengine inafikia hadi kukatika midomo na miguu na maeneo mengineyo ya mwili.

Katika hali hiyo, mambo kadhaa yatakusaidia kuondokana na changamoto za ngozi katika msimu wa baridi na kukufanya kuwa mwenye furaha wakati wote.

**Kunywa maji**

Katika kipindi hiki cha mvua na baridi watu wengi hawana mazoea ya kunywa maji kwa sababu ya hali ya kijibaridi.

Hata hivyo, unatakiwa kujitahidi kunywa maji mengi. Ili kuongeza ladha kwenye maji yako, ongeza limau au ununue maji yenye ladha tofauti.

**Face oil**

Ukimaliza kupaka mafuta au kulainisha ngozi, jipake 'face oil' ili kutunza unyevu unyevu wako na hautahisi ukavu zaidi.

**Usisugue uso**

Wakati wa kipupwe, ngozi inapoteza unyevu kwa urahisi. Ukishindwa kulainisha ngozi yako, unaandaa mazingira mazuri ya ngozi kukauka na utakisikia vizuri.

Tiba ya kusugua uso maarufu kama 'Scrub' fanya mara moja kwa wiki. Usizidishe kwa sababu utasababisha ukavu zaidi.

**Mafuta ya mikono**

Usiache mikono yako ikawa mikavu. Hakikisha unatumia mafuta ya kulainisha viganja na kwenye midomo tumia mafuta ya lip balm na lip jelly.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Supu ya Karoti

SUPU ya karoti ni chakula kizuri kwa afya, lakini ni rahisi kupika wakati ukiwa nyumbani.

Mahitaji

Mafuta ya kupikia, kitunguu maji kilichokatwakatwa, karoti nne, punje tano za kitunguu saumu, mchuzi wa mboga, majani ya giligilani, vijiko 3 vya giligilani ya poda na maji ya limau vijiko 2.

Kungumanga ya poda kijiko 1, chumvi na pilipili nyeusi.

Maelekezo

Osha na ukatekate karoti katika vipande unavyotaka.

Pasha mafuta kwenye sufuria kubwa na kaanga vitunguu maji, karoti na vipande vya kitunguu saumu ulivyokatakata kwa dakika nne.

Mara baada ya kuwa laini, ongeza giligilani ya poda, chumvi na pilipili nyeusi na ukoroge.

Mimina mchuzi wa mboga kwenye sufuria. Funika sufuria na uiruhusu kuchemsha hadi karoti ziwe laini kwa dakika 15.



Koroga kisha ongeza majani ya giligilani, ondoa kutoka kwa moto na uongeze maji ya limau, kungumanga na viungo vinginevyo unavyopenda.

Unaweza kutumia Brenda kuchanganya supu yako.

Supu itakuwa imepoa wakati inachanganywa, kwa hivyo ikiwa unapanga kula mara moja, pasha tena supu bila kuichemka na uitumie.

Ikiwa unaihifadhi kwa ajili ya baadaye, iache ipoe na kuiweka kwenye chombo kisichopitisha hewa kwenye jokofu.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Fahamu sababu zinazochangia nyumba kuvuja muda mfupi baada ya kujengwa



KUWA na nyumba bora na imara ni ndoto na furaha ya kila mtu anayemiliki au anayetarajia kumiliki nyumba hiyo.

Lakini inapokuwa kinyume na matarajio ya kumiliki nyumba ya vigezo hivyo na kukatokea shida ya kiharibika mapema hususani kuvuja, moyo huinama japokuwa wakati mwingine hali hiyo inasababishwa na kukosea uchaguzi wa wataalamu wa ujenzi wa nyumba husika ambao hujenga chini ya kiwango.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Andrew Kitale, anazungumzia sababu mbalimbali zinazochangia baadhi ya nyumba kuvuja muda mfupi baada ya ujenzi wake.

Anasema ziko sababu mbalimbali zinazochangia nyumba nyingi kuvuja ambazo watu wanapaswa kuzifahamu na kuchukua hatua wanapojenga ili kuzuia athari kutokea baadaye.

Kitale anataja miongoni mwa sababu kuu zinazochangia tatizo hilo ni pamoja na matumizi ya vifaa vya ujenzi vya hali ya chini ambavyo baadhi ya watu hufanya hivyo kwa kudhani kuwa wanaokoa pesa.

Sababu nyingine, anasema baadhi ya vifaa vinavyovaliwa na mafundi wakati wa kuezeka huwa sio rafiki kwa paa na hivyo kudhoofisha kifuniko cha paa ambacho baadae hutengeneza ufa na kupitisha maji.

Mbali na sababu hizo, pia anasema paa la nyumba linaweza kuharibiwa na upepo hasa kama halikuezekwa kwa utaalam mzuri na hivyo kuvuja.

Sababu nyingine anasema ni muundo wa paa lenyewe pamoja na makosa yaliyofanywa wakati wa kuezeka na kwamba kwa makosa hayo ya kuvuja kunaweza kutokea hata ndani ya mwaka mmoja baada ya ujenzi wa nyumba husika.

Pia anasema ufungaji mbaya wa paa wakati wa kuezeka ni sababu pia na kwamba kasoro hiyo huonekana haraka ndani ya wiki chache baada ya nyumba kuanza kutumika.

"Paa linaweza kuvuja kwa sababu ya ukiukaji wa matumizi ya teknolojia ya ujenzi. Kwa mfano, kitaalamu unatakiwa kuweka nyenzo za kuezekea katika tabaka tatu, wewe unaweka tofauti na hapo na makosa mengine madogo yanayofanana na hayo yanayofanywa wakati wa kuezeka," anasema.

Anashauri kwamba njia nyingine ya kuepuka paa lako kuvuja ni kuwa makini kuchagua wataalam wa kukuezekea, kutumia vifaa bora bila kujali gharama, kufuata kanuni zote za uezekaji na kukagua paa la nyumba yako mara kwa mara angalau mara mbili kwa mwaka na kuondoa vitu vyote ambavyo hutuama juu yake ambavyo kwa namna moja ama nyingine hutengeneza nyufa hususani vyuma na **vitu** vizito.

DONDOO

Na Restuta James

## Tumia njia hii kupanga jiko dogo



BAADHI ya wasomaji wa ukurasa huu wamenipigia simu kutaka kujua wanawezaje kuweka kila kitu cha msingi kwenye chumba kidogo cha jiko.

Wengine wamezungumzia changamoto wanazokutana nazo kwenye nyumba za kupanga, wamiliki wengi hawatilii maanani umuhimu wa jiko.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa hata jiko dogo, unaweza kupangilia vizuri na kuweka vitu vyote vya msingi.

Akizungumza na Nipashe mapema wiki hii, mtaalamu wa mpangilio wa nyumba na mapambo, Brown Joseph, anaeleza kuwa jambo la msingi ni kuhakikisha kila mita moja ya mraba inatumika ipasavyo.

Anasema mpangilio mzuri utalipa jiko mwonekano maridhawa na 'kuficha' udogo wake wa asili.

1. Kama kuta za chumba hiki hazijabandikwa marumaru, hakikisha unapaka rangi ya kuvutia.

2. Nunua vyombo muhimu tu, kuanzia sufuria hadi sahani. Hii itakuepusha kuwa na vitu visivyotumika.


3. Buni kabati dogo linaloweza kukaa ukutani na kuhifadhi vyombo vichache ulivyonavyo.


4. Meza ya jiko isiwe pana sana, hii itakupa nafasi ya kuweka ua au mmea wa asili kama rosemary.

5. Waweza kuweka kabati dogo ukutani kwa ajili ya viungo vya chakula, hii itakupa nafasi ya kutembea ndani ya chumba hicho.

**Tuwasiliane kupitia 0753 333330**
**restutajames@gmail.com**

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
EEBABA MUONYESHE NJIA HUYU MJA WAKO, HIZI NGUVU ANAZOTAKA KUZITUMIA KULIPIZA KISASI KWA MGONI WAKE AMBAYE 'HAJAMJUA' AZIELEKEZE SHAMBA APATE MAZAO MENGI.
NIKIINUA USO WANGU UTAMJUA
HUYU NI MKE WANGU! TULIKUWA SEBULENI KWETU BAADA YA MECHI YA WATANI NIKASHANGILIA SANA NIKASTUKIA 'NDOSI MOJA' NIKAKATA NETIWEKI, NDIO KUAMKA NAJIKUTA NIPO MBELE YAKO SIJUI NIMEFIKAJE?
MTAALAMU WA KUPIGA VICHWA KAMA HIVYO HAKUNA ALIYEVUNJA REKODI YA MKE WANGU NITAZAME MIMI 'SINA MENO!'
DOKTA


JUKWAANI
'HIVI KWA NINI MECHI ZA WATANI WA JADI SIRIKALI ISIAMUE ZICHEZWE KWA SIRI ILI MWENYE 'KILANGA' AKAYATAFUTE MATOKEO AFE PEKE YAKE?'
HA HA HAAAA! HII ILIYOPITA "BILOKO YA KOLIA" IJAYO SIJUI ITAKUWA NINI JAMANI?
'BOLINGO YA MOTEMA HA HA HAA!'

HABARI KIMATAIFA

# Iran yatuliza wasiwasi, yasema haitalipiza kisasi

**TEHRAN,** IRAN

JOTO la mgogoro kati ya nchi za Iran na Israel, linaelekea kutulia baada ya Iran kuonyesha nia ya kutoendeleza majibizano ya mashambulizi.

Kauli iliyotolewa hivi karibuni na Ofisa wa ngazi ya juu wa Irani kwamba nchi yake haina nia ya kulipiza kisasi baada ya Israel kufanya shambulizi la ndege zisizo na rubani juzi, imeonyesha hali ya wasiwasi imeanza kutulia.

Ofisa wa ngazi ya juu wa nchi hiyo alikaririwa na shirika la habari la Reuters kuwa hawana mpango wa kulipiza kisasi baada ya shambulizi katika mji wa Isfahan usiku wa kuamkia Ijumaa.

Afisa huyo ambaye jina lake halikutajwa, alisema kilichotekea ni hujuma za kujipenyeza na sio mashambulizi kama yanayoripotiwa na vyanzo vya kigeni.

Hata Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Hossein Amirabdollahian, akizungumza na wajumbe wa mataifa ya Kiislamu mjini New York, alisema mashambulizi hayo yalifanywa na ndege na hayakusababisha uharibifu wowote.

Hata hivyo, nchi ya Israel haijatoa taarifa yoyote juu ya mashambulizi, licha ya mshirika wake mkuu, Marekani kukataa kuhusika nyuma ya mashambulizi hayo.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin alifanya mazungumzo na mwenzake wa Israel, lakini taarifa za ndani kuhusu mazungumzo yao ilieleza walijadili namna ya kupunguza mivutano, na bila kuitaja Iran.

Israel imearifu jana kuwa imeongeza juhudi za kuingiza misaada ya kiutu kwa wakazi wa Ukanda wa Gaza.

Katika taarifa yake ilisema malori 276 yaliyobeba chakula na dawa yaliingia ndani ya Ukanda wa Gaza siku ya Alhamisi, kwa mujibu wa mamlaka inayohusika na mawasiliano na Wapalestina, COGAT.

Aidha, paketi 144 za chakula zilidondoshwa kutokea angani, na malori mengine 700 yanasubiri kuingia katika kituo cha ukaguzi cha Kerem Shalom.

Misaada hiyo inachukuliwa na mashirika ya msaada ya Umoja wa Mataifa ya kusambaza chakula.

Kutokana na janga la kibinadamu linalowatishia watu wa Gaza, Israel imekuwa ikikabiliwa na shinikizo kutoka washirika wake wa nchi za magharibi na Umoja wa Mataifa, kuitaka iruhusu haraka kuingizwa kwa shehena zaidi za msaada.

Ingawa mashirika ya wahisani yamethibitisha ongezeko la msaada unaoingia Gaza, yalisisitiza kuwa bado malori yanayoruhusiwa kuingia hayatoshi, na kulaumu mapigano yanayoendelea kuwa kipingamizi.

**DW**



Wanajeshi wa Thailand washika doria katika mpaka wa nchi hiyo na Myanmar baada ya kutokea mapigano jana. **PICHA: AFP**

## Wanajeshi 10 waliokufa ajali ya ndege waagwa

**NAIROBI,** KENYA

VIONGOZI mbalimbali wakiongozwa na Rais wa Kenya William Ruto, wameshiriki katika ibada ya wafu ya makamanda wakuu wa kijeshi iliyofanyika jana katika uwanja wa michezo wa Ulinzi, uliopo ndani ya kambi ya Langata.

Rais Ruto alijumuika na waombolezaji na wanafamilia wa wanajeshi kumi akiwamo mkuu wa majeshi ya nchi hiyo Meja Jenerali Ogolla, waliofariki kwenye ajali ya ndege ya kijeshi iliyotokea alhamisi, Aprili 18.

Katika baadhi ya sherehe hizo ilikuwa tofauti na ibada za kiraia, kwani itifaki na tamaduni za kijeshi ziliandaliwa kwa ajili ya kutoa heshima za mwisho kwa wanajeshi hao. Miili ambayo ilikuwa inahifadhiwa katika hospitali ya kijeshi ye Defence Forces memorial ilisafirishwa hadi uwanjani ambapo majeneza yalifunikwa kwa bendera ya nchi hiyo.

Baada ya kuwasili gwaride la heshima lilifanyika kwa ajili ya kuwapa wanajeshi waliofariki heshima, kisha miili ilizungushwa mzunguko mmoja ndani ya uwanja wakati wanajeshi waliokuwa uwanjani wakipiga saluti ya mwisho kwa marehemu.

**BBC**

## Kambi ya jeshi Iraq yashambuliwa

**BAGHDAD,** IRAQ

MTU mmoja ameuawa na wengine wanane kujeruhiwa kufuatia mlipuko uliotokea katika kituo kimoja cha jeshi la Iraq usiku wa kuamkia jana.

Mlipuko huo ulitokea kwenye kituo cha jeshi cha Kalsu katika jimbo la Babylon, kusini mwa mji mkuu wa Baghdad, ambako kuna vikosi vya wanamgambo wa muungano wa Hashed al-Shaabi.

Tukio hilo limetokea siku chache baada ya Iran kufanya mashambulizi ya kulipiza kisasi dhidi ya Israel, na kisha Israel kulipiza kisasi kwa kuipiga kwa kutumia ndege zisizo na rubani.

Kitengo cha habari cha jeshi la Iraq kilisema mlipuko na moto ulipiga kituo cha Kalsu alfajiri ya Jumamosi, na kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Lakini kamandi ya jeshi la anga ya nchi hiyo, ilisema hakukuwa na dege zisizo na rubani ya adui kwenye anga la jimbo la Babylon kabla na wakati wa mlipuko huo.

Hapo awali, ofisa mmoja kutoka wizara ya mambo ya ndani aliripoti kuwa mashambulizi ya anga yalifanyika katika eneo hilo.

Kundi la Hashed al-Shaabi lilisema kwenye taarifa yake kwamba mlipuko huo ulisababisha hasara kwa watu na mali bila kutoa ufafanuzi zaidi.

Hata hivyo, kundi hilo lilikiri kuwa majengo yake kwenye kituo hicho cha kijeshi yameshambuliwa na kwamba wachunguzi wamepelekwa kwenye eneo hilo.

Aidha, hakuna kundi wala nchi yoyote iliyodai kuhusika na mkasa huo, wala vyanzo vya usalama havikumtaja yeyote vinayemtuhumu kufanya mashambulizi hayo.

Muda mfupi baada ya mlipuko huo, jeshi la anga la Marekani lilisema vikosi vyake havikuhusika na shambulizi hilo.

"Marekani haijafanya mashambulizi ya anga nchini Iraq leo," ilisema Kamandi Kuu ya Marekani (CENTCOM) kupitia mtandao wa kijamii wa X, na kuongeza kwamba taarifa zinazosambaa kuwa wanajeshi wa nchi hiyo wamefanya mashambulizi si za kweli.

Ofisa mmoja wa jeshi la Iraq, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba mlipuko huo ulitokea kwenye ghala la kuhifadhia silaha.

Kwa upande wa Jeshi la Israel, lilieleza kwamba haliwezi kutoa maelezo kwa sababu halizungumzii taarifa zinazochapishwa na vyombo vya kigeni.

**DW**

## MAKALA

# USHAURI BILA MATUSI INAWEZEKANA



Na Magabilo Masambu

**Mivutano inaweza kutumika kama mifupa anayorushiwa mbwa anayemfukuza mwizi na mwisho wa siku, mwizi hatakamatwa na badala yake mbwa ataendelea kuzubaa akila mifupa hiyo ambayo pia ataishia kuilambalamba tu kwa sababu hana uwezo wa kuitafuna.**

SIFA kubwa tuliyokuwa nayo kama nchi ilikuwa juu ya umoja wetu. Majirani na dunia nzima walijua hivyo ndiyo maana wenye shida na nchi zao sisi tulikuwa washauri na wasaidizi wao. Inawezekana bado tu washauri wao lakini nafikiri sasa wanaweza kuwa wanatutazama tofauti.

Tunajenga nchi kwa wanufaa yetu sote na vizazi vyetu ya nini tugombanie fito? Pengine wakati mwingine kutotambua wapi fito na miti iliyojenga nyumba yetu ilikotoka, hilo linaweza kuwa tatizo.

Kuna wakati kutofahamu sawasawa historia ya mafanikio yetu, kunaweza kuzaa laana ambayo inaweza kuwa inatufarakanisha bila kujijua.

Lakini bado naamini tunaweza kusemezana kwa lugha tulizofundishwa kutumia majumbani.

Kuna umuhimu wa kuwa na mawazo jumuishi kwa maana ya kusikiliza kila mtu anasema nini kuhusu sisi au nchi.

Nikubaliane na kauli ya Rais Samia Suluhu aliyowahi kuitoa wakati wa mkutano wake na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa kwamba katika nchi hii hakuna mwenye hatimiliki na kwamba tuishi kwa kuheshimiana.

Ukweli huo unapaswa kuheshimiwa na kila mmoja wetu kwa sababu sheria hazipaswi vilevile kusimamiwa kwa kubaguliwa maana tunaambiwa sheria ni msumeno na kwamba unakata pande zote japo mingi ninayoifahamu ina makali upande mmoja na upande mwingine ni butu. Kwa hiyo inaweza kutumika kukata upande mmoja na kuacha upande mwingine!

Mivutano inaweza kutumika kama mifupa anayorushiwa mbwa anayemfukuza mwizi na mwisho wa siku, mwizi hatakamatwa na badala yake mbwa ataendelea kuzubaa akila mifupa hiyo ambayo pia ataishia kuilambalamba tu kwa sababu hana uwezo wa kuitafuna.

Maana yangu ni kwamba leo tuna zaidi ya miaka 60 ya uhuru na maendeleo tulio nayo leo hatuwezi kujivuna sana japo nakubali kwamba yako mambo yamefanyika katika ujenzi wa miundombinu, elimu, afya na maeneo mengine lakini kusema kweli pengine tusingekuwa na hii mivutano na malumbano ya huyu kamtukana yule na kadhalika, tungalikuwa tumepiga hatua zaidi.

Siku tutakayotambua kwamba kila mmoja katika nchi hii ana mchango katika maendeleo bila kutazama dini, kabila, chama cha siasa anachotoka na kwamba mawazo na jitihada zake zinatumika na kuheshimika, basi tungalikuwa mbali zaidi ya hapa.

Inawezekana tunayo matatizo katika maeneo ya kisheria basi yatazamwe.

Kama ni ya kimaadili yazungumzwe ili mradi turudi pamoja kama taifa moja lenye nia moja ya kujenga nchi. Bahati mbaya tuliyo nayo ni kwamba nia njema inazungumzwa lakini hazitekelezwi.

Yasiyozungumzwa ndiyo hutekelezwa, yasiyotekelezwa ndiyo yanahitajika, wanaoyahitaji hawayazungumzi.

Inawezekana hajapatikana refa anayetakiwa kupuliza kipenga wakati timu mbili zinapokuwa uwanjani.

Kama watu wawili wamekosana au hawaelewani, ni vyema lazima apatikane mtu wa tatu nje ya mahakama za kisheria badala yake ndani ya mahakama za majadiliano ili kusikiliza hoja za pande mbili na kuwaunganisha wawili hawa.

Zamani migogoro mingi katika jamii ilitatuliwa na wazee. Bado naamini wazee hao hawajaisha bado wapo. Iwe migogoro ya kimila, kisiasa au kiserikali wanaweza kusimama kwenye nafasi zao wakashauri kwa sababu kuishi kwingi ni kufahamu mengi. Inawezekana makosa mengine yanatokana na kutoijua historia.

Kauli na vitendo ni mambo mbalimbali.

Zinaweza kutoka kauli nzuri sana kwa viongozi wetu juu ya umoja wetu lakini vitendo vikakinzana na kiukweli hili ni tatizo moja tulilo nalo Afrika.

Tatatizo hili linatokana na utamaduni wa kufundishwa uongo tukiwa wadogo.

Mara nyingi tu inatokea kutoa maelekezo kwa watoto kwamba mtu fulani akija mwambieni sipo nimetoka, wakati umelala ndani.

Kwa hiyo mtoto tayari anafundishwa kusema asichoamini hata mwenyewe maana anafahamu fika upo.

Naamini kwamba siku tutakapoamua kuzitendea haki hotuba zetu na matamko mbalimbali tukayatekeleza kama tunavyoyasema kwenye majukwaa, basi tunaweza kuwa tumetengeneza jambo jema sana ambalo litabaki kwenye historia ya maisha yetu.

Bado tunayo nafasi ya kuwa wamoja pamoja na tofauti za kimtazamo na katika hili si lazima tufikiri sawasawa, kutofautiana ndiyo uhai wetu lakini usitumike kudhalilisha pia utamaduni wetu kama Watanzania.

Kila mmoja anatakiwa kujiona kuwa anayo nafasi sawa ya kujiletea maendeleo yake binafsi na ya nchi kwa ujumla.

Haipaswi kuonekana kwamba wako wanaotakiwa kujenga nchi na wengine wabaki watazamaji. Hilo halitakuwa tofauti na ubaguzi wa aina yoyote ile kama wa rangi na kadhalika na mambo yote haya bado yanaweza kufanyika bila kutukanana na kudhalilishana japo tunayo haki ya kushauri.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kisa cha mwanaume aliyetunukiwa shahada ya uvumilivu wa mapenzi*



Na Adam Fungamwango

**Miaka hiyo jamaa alikuwa mfanyabiashara wa kununua korosho mikoa ya Kusini kwa wakulima na baadaye yeye kuuza kwenye miji mikubwa na hata nje ya nchi.**

KATIKA ya miaka ya 1980, kuna mwanaume mmoja, alitunukiwa shahada ya uvumilivu wa mapenzi.

Waliomtunuku mwanaume huyo ni wanamuziki na mashabiki wa bendi ya DDC Mlimani Park Orchestra.

Wakati wa kumtunukia huko, wakamtungia na wimbo waliouita, 'Shahada ya Uvumilivu.'

Ilikuwa kama 'sapraizi' tu, wakati anaingia ukumbini tu, muziki waliokuwa unapigwa ukakatishwa, na kupigwa wimbo mpya ambao ulikuwa haujawahi kusikika.

Maudhui ya wimbo ule, uliwafanya wengine walie machozi, lakini mwenyewe alipousikia alishangaa na kufurahi kwa wakati mmoja.

Wimbo huo ambao ndiyo ilikuwa ni shahada tosha kwake, ulimfanya kufarijika na kupunguza kabisa maumivu aliyoyapata awali kama si kuyaondoa kabisa.

Alikuwa ni shabiki mkubwa wa bendi hiyo na alikuwa hakosi kwenye maonyesho yao, alifurahi kupita maelezo, miezi michache baadaye, Sikinde wakaenda kuurekodi wimbo huyo kwenye studio za Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) enzi hizo, sasa TBC.

Labda utajiuliza ni kitu gani kilichomtokea jamaa huyo hadi kufikia hatua ya Sikinde kumtungia wimbo?

Miaka hiyo jamaa alikuwa mfanyabiashara wa kununua korosho mikoa ya Kusini kwa wakulima na baadaye yeye kuuza kwenye miji mikubwa na hata nje ya nchi.

Msimu mmoja wa korosho akaamua kwenda na mkewe ili aone ni jinsi gani anavyofanya biashara hiyo.

Walipofika kwenye hoteli moja kubwa kwenye moja ya mikoa ya Kusini, kesho yake jamaa akamuacha mkewe ili kuwafuata wakulima vijijini kununua korosho zao, na akishakamilisha zoezi hilo arejee hotelini alikomuacha mkewe. Aliporudi hakumkuta. Tafuta huku na huku, wapi! Jamaa alichanganyikiwa.

Uliza huku na kule. Ndipo kuna watu hapo hapo hotelini walipomtonya kuwa aliondoka na mtu mwingine na walionekana kuwa na tahadhari sana.

Baadaye ikagundulika kuwa alirubuniwa na mwanaume mwingine ambaye alifika hapo, alipomuona anampenda, akamtongoza na kumpa maneno mengi matamu kama asali na laini kama sufi.

Ubuyu wote sasa ukawa mikononi mwake. Akaondoka na shehena yake ya korosho kwa ajili ya biashara, lakini hakurejea kwa mke. Hili lilimtesa kiasi cha kuhadithia rafiki zake wa karibu, akiwemo mtunzi wa wimbo huo, Benovilla Antony.

Msimamo wa jamaa ni kumuachia Mungu. Akaapa hatolipiza kisasi chochote, na anaendelea na maisha mengine ingawa roho ilimuuma sana.

Kisa hicho Benovilla alikichukua na kukitengenezea wimbo ambao baada ya kukamilika ulipigwa kwa mara ya kwanza akiwa anaingia ukumbini na kumshangaza sana.

Mkasa mzima wa tukio unasimuliwa na wimbo huu uliotwa 'Shahada ya Uvumilivu.'

"Habari zako tumezisikia, ewe jirani yetu Moyogani eee, tulijua toka zamani kwamba, mama Hadija ni malkia katika nyumba yako.

Hakuna kilichokuwa chini ya uwezo wako akakikosa Moyogani eee, kwa hakika mkataa pema pabaya panamwita, ooh jirani, kweli huna lawama."

Hapa Benovilla amejinasibisha kama jirani wa Moyogani, akiwa anafahamu matunzo yote ambayo jamaa anampatia mkewe, lakini ikawaje?

"Akatokea hasidi mvurugaji wa mambo, kamshawishi mkeo mama Hadija, akufanyie vituko kusudi umwache arudi kwao, baadaye aende kwa hasidi Nachingwea. Huko akaolewe kwa mkataba wa kujengewa nyumba yao, eee uchungu wa jambo hili ni mkubwa, lakini ulivumilia."

Ni kawaida ya wanamuziki, wakipata kisa cha kweli, watapunguza baadhi ya vitu, wataongeza vingine ili mradi kuongeza ladha ya maudhui yanayokubalika kwa jamii.

"Nia yetu ni kukuasa, uendelee na uvumilivu jirani yetu, tena sote twakusubiri, Sikinde Ngoma ya Ukae, tukutunukie shahada ya uvumilivu."

Wala wewe ulipize kisasi kwa hasidi aliyemrubuni mkeo, mwache acheze na pesa, dunia itamchapa, itamchapa viboko, Moyogani eee.

Tunajua ulipatwa na uchungu kwa pande zote mbili, lakini uliheri kulala juu ya paa, kuliko ndani ya nyumba, iliyokanganyika, Moyogani ee." Huyo ndiye mwanaume pekee aliyewahi kutunukiwa shahada wa uvumilivu wa mapenzi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

UMBILE la msichana huyo lilimshtua. Licha ya kuonyesha hakuwa na maisha bora, hata nguo tu alizokuwa amevaa, lakini aliweza kuwazidi hata wale wasichana wanaoshinda saluni.

Hilo halikuonekana sana kwenye macho ya kawaida. Ilibidi mtu mwenye jicho la tatu kuweza kutambua kuwa iwapo atatunzwa vyema, atakuwa mrembo mara kumi ya alivyo.

"Ahsante kaka." Heri alishtuliwa na shukrani kutoka kwa binti huyo.

"Usijali dada yangu. Unaitwa nani?"

"Naitwa Nuru.", akaitikiwa kwa sauti tulivu na ya upole. "Mhh! Na kweli Nuru." Akasema Heri na kusababisha binti wa watu kutabasamu.

Tayari Heri na Nuru walishaanza kuvuta hatua kadhaa kutoka dukani na sasa walikuwa wanatembea wakiwa wawili.

"Unaishi wapi?" Heri akauliza tena "Hapa hapa Chanika, wala siyo mbali, nyumba hizo za nyuma hapo."

"Unaishi na nani?" Bado maswali yalikuwa yanafululiza kutoka kwa Heri.

"Shangazi," akajibu. Heri hakutaka kumwambia chochote kwa jinsi alivyotokea kumpenda ghafla.

"Naomba namba yako ya simu, kwa sasa nina haraka sana, ninahitaji kuongea na wewe."

Nuru akajaribu kumtazama usoni Heri, lakini akashindwa kutokana na aibu, akarudisha kichwa chini, akamwambia, "sina simu."


Ilimchanganya kidogo Heri kiasi cha kutojua kama ni kweli, au ananyimwa namba kwa makusudi.

Mawazo yote mawili alikuwa nayo. Labda ananyimwa tu kwa sababu msichana huyo hakuwa tayari, hajampenda licha ya msaada wake, au ana mwanaume hivyo anaogopa kuonekana ana namba ya mwanaume mwingine kwenye simu yake.

Pili kwa jinsi alivyomuona msichana na jinsi alivyokuwa wakiongea na muuza duka, maisha yake yaliionyesha huenda ni kweli hakuwa na uwezo wa kumiliki simu.

Kuna wakati akili ilimwambia wapo wasichana kama yule na aina ile ile ya maisha, lakini wana simu za mkononi, tena za bei mbaya.

"Wananunuliwa." Akajijibu mwenyewe. "Na nani?" Akajiuliza. "Na mabwana zao." Akajijibu. "Huyu hana bwana?" Akajiuliza tena. Mwisho akaamua tu kuituliza akili yake na




**"Wananunuliwa." Akajijibu mwenyewe. "Na nani?" Akajiuliza. "Na mabwana zao." Akajijibu. "Huyu hana bwana?" Akajiuliza tena. Mwisho akaamua tu kuituliza akili yake na ikubali tu kuwa hana simu, vinginevyo atajiuliza na kujijibu maswali mengi mpaka kichwa kitamuuma.**

ikubali tu kuwa hana simu, vinginevyo atajiuliza na kujijibu maswali mengi mpaka kichwa kitamuuma.

"Sasa tutawasiliana vipi? Tunaonana wapi? Nina mengi tu mazuri ya kukwambia."

"Si uniambie tu hapa hapa?"

"Nina mengi tutakaa sana na si kijuujuu hivi."

"Basi mimi napeleka mchele huu kwa shangazi, niambie nitakukuta sehemu gani?" Nuru alitoa nafasi kwa Heri.

Lilikuwa ni kosa la kiufundi. Ndicho alichokuwa akihitaji. "Utanikuta pale mbele kwenye mgahawa pale, nje wanauza juisi na soda, nitakuwa nakunywa juisi nakusubiri."

"Haya, we nenda, napeleka hivi vitu, namuaga shangazi mara moja nakuja."

Ilipita kiasi cha saa nzima Heri hakuona mtu yeyote anayefanana na Nuru akija. Alimaliza juisi akaagiza na nyingine, lakini wapi.

Kiasi cha saa moja na dakika 10 kupita tangu walipoachana barabarani, ndipo alipomuona Nuru akiangaza macho akitafuta anayemhitaji kwenye mgahawa.

"Nipo hapa." Nuru alisikia sauti ya Heri, akaenda kukaa kwenye kiti kinachoangalia naye ambacho kilitenganishwa na meza. Zile hasira zake alizokuwa nazo baada ya kukwekwa na zaidi ya saa moja, zilifutika alipoiona tena sura ya Nuru.

"Agiza unachotaka." Muda huo alikuwa mhudumu. Akaagiza chips na mishikaki miwili.

Heri akaongeza na maji. Si kwamba alikuwa na pesa nyingi. Ila alitumia na za ziada kwa nia tu ya kumpata msichana yule.

Wakati akiendelea kula, ndipo Heri alipotoa la rohoni. Akamwambia jinsi alivyotokea kumpenda, pindi tu alipomuona.

Mazungumzo baina yao yalikwenda sawa. Yalikwenda kama alivyohitaji Heri. Na wakakubaliana kuonana baada ya wiki moja.

"Uje nyumbani kwangu. Ukipanda gari hapa kama unakwenda Zingiziwa, kituo cha kwanza ukishuka, kuna njia barabara ya vumbi, ukienda nayo hiyo mbele kuna duka upande wa kushoto, utakata kulia, njia hiyo hiyo nenda nayo, utakuta nje kuna kioski cha juisi ya miwa, Walivyokubaliana na kwamba akifika eneo ambalo alimwambia kuna kibanda kinachouzwa juisi ya miwa, mbele yake atakuta mlango ambao hufungwa muda wote, lakini siyo kwa komeo hadi saa tatu usiku unakuwa wazi."

Wakaelekezana wakaelewana, ambapo muda waliopatana ulikuwa ni saa 10:00 jioni.

********************************

Mlio mkali uliomshtua Heri kutoka kwenye lindi la mawazo. Alipoangalia ni nini, macho yake yalikutana na bakuli lililoanguka kutoka kwenye beseni. panya mmoja aliyepita juu ya beseni hilo, alisababisha lianguke na kutoa mlio huo uliomshtua kutoka kwenye lindi la mawazo.

Ndipo alipogundua kuwa bado yupo kitandani. Anamsubiri mgeni wake Nuru aliyemuahidi atakuja nyumbani wake.

Bado harufu kali ya panya iliendelea kupenya kwenye matundu mawili ya pua zake. Hapo akakumbuka pia kuwa moja ya kazi zilizomfanya hadi kufikia hatua ile ni kumsaka panya aliyekufa ili mpenzi wake ambaye ni mara ya kwanza kufika pale, asikutane na harufu ile.

Akakumbuka kuwa ameshatafuta sana bila mafanikio, mwisho akaamua kukaa kitandani.

Akaangalia saa yake, ilibaki kiasi cha dakika 20 hivi kufika saa 10:00 kamili. Akili yake ikamtuma saa kukimbia. Afunge mlango na kuondoka ili Nuru akija asimkute. Dakika moja baadaye akaona halikuwa wazo la busara kwa sababu lingeweza kusababisha kumkosa kabisa Nuru kwani angeonekana si tu kwamba muongo, lakini hajali.

Akawaza kitu kingine kabisa. Akatabasamu. "Ndiyo, hapa sasa tatizo litakuwa limeisha." Akajisemea mwenyewe huku akipiga ngumi za ushindi hewani.

Presha ikamshuka, furaha ya kutembelewa na mpenzi ikarejea tena. Mwanzoni aliona dakika chache tu zimebaki kabla hajafika, lakini kwa sasa aliziona ni nyingi.

Wazo la kumsaka panya aliyekufa likafa kabisa.

Kwa sababu ameshafanya hivyo zaidi ya masaa mawili bila mafanikio. Sasa alikuwa na wazo la njia mbadala ili kupoteza harufu ya panya ili isimkere mgeni wake.

Alikuwa na uhakika kitu alichokiwaza kukifanya ili kupoteza harufu ya panya kitafanikiwa na ilikuwa ndiyo njie pekee iliyobaki kwa muda huo.

Akachukua shilingi elfu moja iliyokuwa mezani, akaiweka kwenye mfuko wake na pensi aliyovaa.

Akaangalia tena saa yake, zilibaki dakika 15 tu.

Tayari kwake zilikuwa ni nyingi hata akifikiria mara nyingi kuna ahadi zinazoitwa za kiswahili. Alijua huenda kuna dakika tano au 10 zingine za ziada kabla mgeni wake hajaingia.

Zilitosha kabisa kutoka na kwenda kuchukua kitu ambacho aliamini ndiyo mwarobaini wa harufu hiyo ya panya chumbani mwake.

ITAENDELEA JUMAPILI



# Diamond, Ziiki kimeumana

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz na kampuni ya kuuza muziki kidijitali Ziiki wameingia katika mgogoro baada ya pande hizo mbili kushindana muda wa kuutoa wimbo mpya wa lavalava.

Diamond alikaririwa akilalamika kuwa kampuni hiyo imeshindwa kufuata kalenda yao ya wimbo huo kutambulishwa Aprili 19, badala imepanga kuuweka hewani Mwezi Mei jambo ambalo kwake ameliona sio sawa.

Hata hivyo, katika taarifa ya Ziiki iliyowekwa mtandao imeeleza kuwa lebo ya wasafi inayomsimamia lavalava, haikufuata utaratibu unaojulikana duniani kote wa kuutambulisha wimbo baada ya wiki tatu tangu ulipowasilishwa katika kampuni hiyo.

Ziiki ikaeleza kwamba kimsingi upande wao hawana kosa kwani wanafuata taratibu zote zilizopangwa kwa ajili ya kuuweka hewani wimbo huo.

# WASANII WAMLILIA GARDNER G HABASH

WASANII wengi wa muziki na filamu wametuma salamu za rambirambi kufuatia kifo cha mtangazaji mkongwe na baba mzazi wa mwanamuziki nchini Malkia Kareen

Gardner alikuwa akifanya kazi katika kituo cha redio cha Clouds FM, alifariki dunia jana wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya moyo ya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam.

Taarifa ya kifo chake ilithibitishwa na kituo hicho, ikieleza Habash alilazwa hapo baada ya kupata matatizo ya shinikizo la moyo.

Katika kurasa zao za mitandao ya kijamii, wasanii maarufu waliandika jumbe mbalimbali za kuonyesha wamehuzunishwa na kifo hicho kutokana na Gardner kuwa mmoja wa watu walionyanyua sanaa ya muziki wakati akiwa hai.



## ZISIKUPITE

### ZIDANE AITAMANI UNITED

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anafuatilia kwa karibu hali ya Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag na angependelea kutua Old Trafford badala ya Bayern Munich. (**L'Equipe, via Get French Football News**)

### BAYERN YAMKANA ZIDANE

KLABU ya Bayern Munich haijawasiliana na mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa, Zinedine Zidane, kuhusu kumrithi, Thomas Tuchel, ambaye anaondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu. (**ESPN**)

### RANGNICK ATAJWA UNITED

ALIYEKUWA Kocha wa Manchester United, Ralf Rangnick, ambaye kwa sasa anaifundisha wa Austria, amejadiliwa na uongozi wa Bayern Munich, huku kocha Brighton Roberto de Zerbi, pia akiwa katika orodha yao ya walimu wanaotajwa katika nafasi hiyo. (**Sky Sport Germany**)

### SANCHO KUITAJIRISHA UNITED

KLABU ya Manchester United inaweza kuwa katika mstari wa kupokea pauni milioni 3.4 za ziada kwa ajili ya mkopo wa winga wa England, Jadon Sancho kwenda Borussia Dortmund ikiwa timu hiyo ya Ujerumani itatinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. (**Times**)

### BRUNO KUBAKI NEWCASTLE

KIUNGO wa kati wa Newcastle United na Brazil, Bruno Guimaraes, mwenye umri wa miaka 26 amedokeza ana nia ya kubakia katika klabu hiyo msimu katika ujao.(**Telegraph**)

### MAATSEN ANOGEWA DORTMUND

MLINZI wa kushoto wa Uholanzi, Ian Maatsen, mwenye umri wa miaka 22, ameiambia Chelsea anataka kuondoka huko na ameonyesha nia ya kusalia Dortmund, ambako yupo kwa mkopo. (**Sky Sport Germany**)

### UNITED, ATLETICO VITANI

KLABU ya Manchester United inakabiliwa na ushindani kutoka Atletico Madrid kuwania saini ya beki wa kati wa Nice na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Jean-Clair Todibo, mwenye umri wa miaka 24. (**Mirror**)

### DE JONG ANUKIA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 26, ambaye anaweza kugharimu kati ya euro milioni 60 hadi 70.(**Relevo**)

### VINICIUS KUTUA FULHAM

KLABU ya Fulham iko tayari kwa ajili ya ofa ya mshambuliaji wa Brazil, Carlos Vinicius, mwenye umri wa miaka 29, ambaye ana mkataba wa mkopo katika klabu ya Galatasaray ya Uturuki hadi mwisho wa msimu. (**Standard**)

### SPURS YAMTAKA WILLIAMS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia mshambuliaji wa Athletic Bilbao mwenye umri wa miaka 21, Nico Williams, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 42.8 katika mkataba wake. (**Telegraph**)

### JOELINTON KITAELEWEKA

MAZUNGUMZO ya Newcastle United na kiungo wa kati wa Brazil, Joelinton yanaendelea vyema na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anakaribia kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Tyneside. (**Telegraph**)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# ZIDANE AKANUSHA KUTETA NA BAYERN

**Kutofahamu Kijerumani na Kiingereza kwa ufasaha vyatajwa ni...**

**MUNICH,** Ujerumani

ZINEDINE Zidane hajawasiliana na Bayern Munich kuchukua nafasi ya Kocha, Thomas Tuchel, atakapoondoka mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa ESPN.

Zidane, mshindi mara tatu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa utawala wake akiwa anaiongoza Real Madrid, amekuwa akihusishwa na jukumu hilo katika vyombo vya habari vya Hispania katika siku za hivi karibuni, lakini vyanzo vilisisitiza kwa ESPN hakuna mazungumzo yoyote yaliyofanyika.

Uwezekano wa mshindi huyo wa Kombe la Dunia la mwaka 1998 kuzingatiwa kushika nafasi hiyo uliongezeka juzi wakati Julian Nagelsmann, ambaye inasemekana alikuwa katika mazungumzo ya juu ya kurejea kwa wababe hao wa Bavaria kama kocha mkuu baada ya kutimuliwa Machi, mwaka jana alipoongeza mkataba wake wa kuinoa Ujerumani hadi mwaka 2026.

Vyanzo vya habari vilisema Zidane yuko katika orodha ya wanaowaniwa na Bayern Munich, akiwa nyuma ya Roberto De Zerbi wa Brighton, Kocha wa Austria, Ralf Rangnick na Sebastian Hoeness wa Stuttgart.

> **Zidane mwenyewe hajashawishika na wazo la kuinoa Bayern Munich, vyanzo vilivyoongezwa kwa ESPN, haswa kutokana na kizuizi cha lugha.**

Mfaransa huyo hawezi kuzungumza Kijerumani wala Kingereza kwa ufasaha, na anaona mawasiliano ni muhimu kwa mafanikio yake.

Hata hivyo, wakala wa Zidane, Alain Migliaccio, yuko karibu sana na rais wa heshima wa Bayern Munich, Uli Hoeness.

Zidane hajafundisha tangu mwisho wa kibarua chake cha pili huko Madrid katika msimu wa joto wa 2021.

Mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa waliyoshinda Madrid mwaka 2016, 2017 na 2018 yamebakia kuwa tukio pekee katika zama za kisasa za mashindano hayo ambapo timu imetwaa ubingwa.

Tuchel anatarajiwa kuondoka mwishoni mwa msimu huu baada ya kampeni mbaya ambayo imewafanya kushindwa kushinda taji la Bundesliga baada ya miaka 11 ya utawala.

Hata hivyo, wamefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kuwatoa Arsenal.



# CANCELO AUMIA FAMILIA YAKE KUTISHIWA KIFO

**BARCELONA,** Hispania

JOAO Cancelo amefichua ukubwa wa unyanyasaji aliopata katika mitandao ya kijamii baada ya Barcelona kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Paris Saint-Germain katikati ya wiki, ikiwa ni pamoja na familia yake kutishiwa kifo.

Barca waliongoza mabao 3-2 kutoka kwa mkondo wa kule Paris lakini walipoteza 4-1 Jumanne walipotoka kwenye kinyang'anyiro hicho katika hatua ya robo fainali.

"Watu walinitishia," alisema Cancelo katika mahojiano na ESPN kabla ya safari ya Real Madrid kwenda katika mechi ya El Clasico itakayochezwa leo.

"Kuna maoni katika Instagram yakimtakia kifo binti yangu ambaye bado hajazaliwa. Hawangeniambia uson, kwa sababu tungekuwa na shida, lakini kwenye maoni wanaandika wanachotaka.

"Wanakera, binti yangu, mtoto wetu ambaye hajazaliwa, ni ulimwengu katili na lazima ujue jinsi ya kuishi nao, najua, lakini sijui niseme nini tena.

"Kumtakia mtoto kifo ni jambo la kusikitisha sana. Watu hawafikirii kuhusu mtu nyuma ya mwanasoka wanayemwona kwenye televisheni. Sisi ni binadamu pia. Sisi ni sawa tu."

Cancelo mwenye umri wa miaka 29, alikuwa mmoja wa wachezaji waliokosolewa baada ya Barca kufungwa na PSG kwa sababu ilikuwa ni kosa lake kwa Ousmane Dembélé ambalo lilipelekea timu hiyo ya Ufaransa kufunga bao la tatu usiku kwa penalti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno pia alijibu maoni yaliyotolewa na mlinzi wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand, ambaye alisema Cancelo, "alikuwa mjinga, mjinga na kama mchezaji mchanga asiye na uzoefu katika hali ya kituo cha hofu."

"Ferdinand alikuwa mchezaji mzuri, lakini nina uhakika alifanya makosa pia," aliongeza Cancelo.

"Sote tunafanya. Lakini bila shaka, ni kazi yake, yeye ni mchambuzi na ana haki ya kusema anachofikiria.

"Ninakubali, ni maoni yake. Labda jinsi nilivyotoa penalti hiyo ilikuwa ni kosa la kitoto, lakini kwa jinsi mchezo ulivyokuwa, kichwa changu kwa sasa, nakubali kukosolewa."

Hata hivyo Cancelo, ambaye yuko kwa mkopo Barca kutoka Manchester City, alisema kudhulumiwa kwa familia yake ni suala tofauti kabisa.

"Kosoa maonyesho yangu, sijali, lakini usizungumze kuhusu familia yangu.

"Imekuwa wiki ngumu sana kusema ukweli. Tulikuwa na shauku ya kufika mbali kwenye Ligi ya Mabingwa. Nafikiri klabu hii inastahili, lakini ni wiki tunapaswa kuondoka."

# Guardiola: Palmer aliomba kuondoka

**MANCHESTER,** England



COLE Palmer alijaribu kuondoka Manchester City "kwa misimu miwili" kabla ya kujiunga na Chelsea, Kocha, Pep Guardiola, amesema.

Palmer alihamia Stamford Bridge kwa dili la pauni milioni 42.5 msimu wa joto na amekuwa mmoja wa waliosajiliwa msimu huu baada ya kufunga mabao 23 katika michuano yote, yakiwamo 20 katika Ligi Kuu England.

Guardiola alishtuka alipoulizwa kama lilikuwa kosa kumruhusu Palmer kuhama lakini akasema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alitaka kuondoka kwenye Uwanja wa Etihad muda mrefu kabla ya kujiunga na Chelsea.

"Ni mchezaji wa kipekee," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilisema mara nyingi, sikutoa dakika ambazo labda alistahili na sasa yuko Chelsea. Ninaelewa kabisa.

"Ni mtu mwenye aibu na mwenye uwezo mkubwa. Ndivyo alivyo. Anacheza kwa kiwango cha ajabu kwa hivyo niseme nini? Uamuzi umefanywa kwa sababu nyingi.

"Alikuwa anaomba misimu miwili aondoke na nikasema abaki. Alisema anataka kuondoka. Tungefanya nini? Nikasema abaki kwa sababu Riyad Mahrez, hayupo, lakini kwa misimu miwili alitaka kuondoka."

# Chelsea yatuma ofa kwa Onana

**LONDON,** England

CHELSEA imepania kuipiku Barcelona katika mbio za kumsajili, Amadou Onana, na tayari wamewasilisha ofa kwa Everton, kwa mujibu wa ripoti.

Onana mwenye umri wa miaka 22 anahusishwa mara kwa mara na kuondoka Goodison Park huku kukiwa na matatizo ya kifedha ya The Toffees na tishio kubwa la kushushwa daraja kutoka Ligi Kuu England.

Barcelona imetajwa inaweza kumnasa kiungo huyo, lakini Barcelona inadai inakabiliwa na vita kubwa ikiwa inataka kumsajili msimu huu wa joto.

Deco, Mkurugenzi wa Michezo wa Barcelona, anasemekana kumtambua Onana kama anayefaa zaidi kwa safu ya kiungo anayotaka kuleta msimu huu wa joto - mchezaji mwenye nguvu ambaye ana uwezo mkubwa wa kumiliki mpira - lakini klabu hiyo haiwezi kulipa pauni milioni 60 inayotakiwa na Everton.

Kwa hiyo Barcelona inajaribu kubuni mbinu za kusajili wachezaji aina ya Onana, lakini inatarajia klabu za Ligi Kuu England zitamnasa.

Bado Onana anaweza kuuzwa pamoja na beki wa kati Jarrad Branthwaite, ambaye anatakiwa na Manchester United.



Wakati wakiwa katika ulimwengu mzuri Everton wangepigana vikali kuwabakisha wawili hao, wanakubali lazima wauze 'mali zao' muhimu ili kupunguza mzigo wa kifedha wa klabu.

# RIADHA AFRIKA MASHARIKI SASA KUFANYIKA ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MASHINDANO ya riadha ya Afrika Mashariki na Kati (EARA) sasa yatafanyika Zanzibar Aprili 26 na 27, mwaka huu badala ya Tanzania Bara kama ilivyotangazwa awali, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha Zanzibar (ZAF), Muhidini Yassin, alisema mashindano hayo yatashirikisha timu za taifa za wanariadha wenye umri chini ya miaka 18 na miaka 20.

Yassin alisema wanachama wa nchi zote 11 za ukanda huo wanatarajiwa kushiriki katika mashindano hayo na wataanza kuwasili Visiwani hapa kuanzia April 24, mwaka huu.

Alisema wenyeji tayari wamejipanga kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa ufanisi na kwa kufuata taratibu za michuano hiyo za kimataifa.

Kuhusu wanariadha wa Zanzibar, alisema tayari wameshachagua vijana 40 watakaounda timu mbili za taifa na wameshaanza maandalizi.

"Zanzibar kuwa mwenyeji wa mashindano hayo kutatupa faida nyingi ikiwemo kuibua vipaji vya vijana na yatainua uchumi wananchi kwa sababu timu ambazo zitafika hapa zitalala katika mahoteli na kulipia kodi," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza pia kuhamishia mashindano hayo Zanzibar kumetokana na ushirikiano uliopo na viongozi wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT).

"Wenzetu wa Tanzania Bara walipata changamoto ya uwanja, na kwa sababu viongozi tuna ushirikiano na umoja mzuri, hawakusita kuyaleta mashindano haya Zanzibar, tunatarajia kuwa na mashindano bora, maandalizi yake yako katika hatia za mwisho," aliongeza.



Shabiki wa Yanga akiwa amejipamba kwa maua akiingia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa tayari kushuhudia mechi ya watani wa jadi iliyochezwa jana jioni katika uwanja huo. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Azam yaanza usajili mapema

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha haitaki kupigana vikumbo kugombea wachezaji baada ya msimu kumalizika, Azam FC imeanza mchakato wa usajili mapema na tayari imetangaza kumnasa beki, Yoro Mamadou Diaby, kutoka Mali, ambaye pia ni mahiri katika ufungaji mabao.

Taarifa iliyotolewa na Azam jana imesema imemsajili mchezaji huyo kutoka katika Akademi ya Yeleen Olympique na ataanza kuonekana rasmi katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Azam imesema mchezaji huyo anayecheza beki wa kati alikuwa wakiichezea Stade Malien de Bamako kwa mkopo.

"Yoro amezichezea timu zote za vijana za taifa za Mali, kuanzia ile ya U-17, U-20 na U-23, na atajiunga rasmi na Azam FC kuanzia msimu ujao wa 2024/2025," iliandika taarifa hiyo.

Akiwa Stade Malien, alisaidia timu hiyo kufika robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu, akifunga mabao katika mechi zote mbili za hatu hiyo dhidi ya Dreams FC ya Ghana, ingawa timu yake iliondolewa kwa jumla ya mabao 3-2.

Rekodi zinaonyesha katika mechi ya kwanza ya robo fainali, ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Machi 26, mwaka huu alifunga bao na matokeo yakimalizika kwa Stade Malien kuchapwa mabao 2-1 na mechi ya marudiano iliyochezwa kwenye Uwanja wa Baba Yara, Ghana Aprili 7, mwaka huu, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, Yoro akifunga tena bao dakika ya 59, kabla ya Sylvester Simba kusawazisha dakika ya 90.

## Mlandege, KMKM FC zapeta Kombe la ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mlandege imetinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la ZFF baada ya kuwachapa Inter Zanzibar FC mabao 4-0 wakati Uhamiaji FC wakiwaondoa Black Sailor kwa kuwafunga magoli 2-0.

Kocha wa Inter Zanzibar FC, Omar Seif, alisema sababu kubwa iliyopelekea timu yake kushindwa kufanya vizuri ni kutoelewana kwa safu ya ulinzi.

Seif alisema kipindi cha kwanza wachezaji wake walicheza vizuri lakini baada ya kufungwa bao moja walitoka mchezoni na kutoka katika mfumo wa kiuchezaji aliowaandaa.

" Mipira yote tuliyowashambulia wapinzani wetu haikuzaa matunda kutokana na washambuliaji kutoelewana vyema, kupoteza umakini hasa katika upande wa kushoto na ndio maana magoli yote tuliyofungwa ni yale yale ya aina moja na yametokea upande huo huo wa kushoto," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Mlandege, Hassan Ramadhani, alisema mbinu na mfumo aliotumia ndio ulipelekea timu yake kupata ushindi huo mnono.

"Kipindi cha kwanza hatukufanikiwa kutawala mchezo sana, lakini kipindi cha pili tulibadilika na hatukufanya makosa," alisema Ramadhani.

## Bingwa kuogelea kupatikana leo

**Na Shufaa Lyimo**

ZAIDI ya waogeleaji 100 kutoka mikoa mbalimbali nchini wanatarajiwa kushiriki mashindano ya Klabu Bingwa ya mchezo huo yatakayomalizika leo kwenye bwawa la kuogelea la Shule ya Kimataifa Tanganyika (IST) jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Habari wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Sebastian Kolowa, alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu 11 kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar na nyingine moja kutoka Nairobi, Kenya.

Kolowa alisema mashindano hayo yamepata baraka za Chama cha Dunia cha Kuogelea na waogeleaji watakaofanya vizuri watapata tiketi ya kushiriki michuano ya dunia itakayofanyika baadaye mwaka huu huko Burgaria.

"Ushindani utachagizwa kutokana na kuwapo na waogeleaji wa kimataifa, Sophia Latif na Hilal Hilal, tunatarajia mashindano yatakuwa na upinzani mkubwa, tunakaribisha wadau mbalimbali wajitokeze," alisema Kolowa.

Kiongozi huyo alisema kila klabu iliyothibitisha kushiriki mashindano hayo ya mwaka huu imejipanga kufanya vizuri kutokana na maandalizi ya muda mrefu waliyofanya.

Michezo
Jumapili Aprili 21, 2024
Nipashe



## Zidane akanusha kuteta na Bayern

UK. 21



Picha kulia: Mshambuliaji wa Yanga, Joseph Guede (kushoto), akipambana kumtoka, Sadio Kanoute wa Simba katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Picha kushoto: Straika wa Simba, Kibu Denis (kulia), akijipanga kumtoka kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAENDELEZA UBABE KWA SIMBA

## Harufu ya ubingwa wa tatu mfululizo yaanza kunukia Jangwani...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO yaliyofungwa na nyota ambaye yuko katika kiwango cha juu, Stephane Aziz Ki na Joseph Guede yalipa Yanga ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wapinzani wao wa jadi Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam jana.

Yanga imeweka rekodi ya kushinda mechi mbili kwa msimu mmoja baada ya misimu minane kupita.

Mara ya mwisho kati ya timu hizo mbili kushinda katika mechi ya dabi ilikuwa ni msimu wa 2015/16, ambapo Yanga iliifunga Simba mabao 2-0 katika mechi zote mbili katika msimu huo.

Mechi ya mzunguko wa kwanza Yanga ilishinda mabao 2-0, yaliyowekwa wavuni na Amissi Tambwe na Malimi Busungu na mzunguko wa pili ilishinda idadi hiyo hiyo ya magoli yaliyofungwa na Donald Ngoma na Tambwe.

Imejirudia tena msimu huu, katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyofanyika Novemba 5, mwaka jana mabingwa hao watetezi walipata ushindi mnono wa mabao 5-1.

Kocha Mkuu wa Yanga, raia wa Argentina, Miguel Gamondi, naye anaingia katika kitabu cha kumbukumbu cha mwalimu aliyeiongoza timu hiyo kushinda dabi mbili kwa msimu mmoja, huku Abdelhak Benchikha, ikiwa ni dabi yake ya kwanza, ambayo ameanza kwa kipigo.

Ushindi wa jana umeifanya Yanga kufikisha pointi 58 na kuukaribia ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo huku Simba ikibakia na pointi 46, lakini imecheza mechi moja pungufu ukilinganisha na vinara hao.

Simba itabidi ijilaumu kwa kukosa mabao mengi ya wazi kwa sababu wao ndio walianza kufika katika lango la Yanga dakika ya pili tu kupitia, Saido Ntibazonkiza, alipopata mpira kwenye wingi ya kulia peke yake, baada ya Joyce Lomalisa kuteleza, lakini alikuwa na papara, badala ya kuangalia wenzake akapiga krosi fyongo iliyodakwa kwa urahisi na kipa, Djigui Diarra.

Yanga ilijibu shambulio hilo dakika moja baadaye, kwa Aziz Ki, kupiga mpira wa mbali kiasi cha mita 40 hivi, baada ya kuona kipa wa Simba, Ayoub Lakred, amesogea mbele ya lango, lakini mpira huo ulitoka juu ya lango.

**Sadio Kanoute kama angekuwa makini angeweza kuipatia Simba bao dakika ya sita kufuatia krosi ya Israel Mwenda iliyotua kichwani kwake, akashindwa kuchagua engo sahihi, badala yake akapiga mpira uliodakwa kirahisi na Diarra.**

Kwa mara nyingine tena, Kanoute alikosa bao akiwa yeye na wavu, dakika ya saba, akipiga mpira pembeni ambao ulirudishwa kimakosa na mabeki wa Yanga.

Moja ya tukio ambalo si la kawaida ni wachezaji wawili wa timu zote mbili, ambao ni raia wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo (DRC), kushindwa kuendelea na mechi kutokana na kuumia.

Lomalisa, beki wa kushoto, aliumia dakika ya sita kwa upande wa Yanga, nafasi yake ikachukuliwa na Nickson Kibabage, na dakika tano baadaye, Henock Inonga, wa Simba, naye alipatwa na tatizo la misuli kama mwenzake, akatoka na nafasi yake ikachukuliwa na Hussein Kazi, ambaye ndiye aliyesababisha penalti iliyozaa bao la kwanza kwa Yanga.

Awali aliokoa mpira ambao ulimbabua Aziz Ki, aliyeuchukua kumfungasha 'tela', kabla ya kucheza madhambi ndani ya eneo la hatari.

Penalti hiyo iliwekwa wavuni na Aziz Ki mwenyewe dakika ya 19, licha ya Lakred kuruka upande sahihi, lakini mpira ulikuwa na kasi zaidi kuliko yeye na kutinga wavuni.

Simba ilikosa tena bao la wazi dakika ya 35, pale Saido alipopata mpira ndani ya eneo la 18, akapiga shuti lililowababatiza mabeki wa Yanga, ukamrudia Kibu Denis aliyepiga shuti lililotoka nje ya lango.

Dakika mbili baadaye, Yanga iliifundisha Simba jinsi ya kutumia nafasi ilipopachika bao la pili, likifungwa na Guede, ambaye akipokea mpira mrefu uliopigwa kutoka katikati ya uwanja, akaumiliki na kuwaacha mabeki wa Simba walidhania ameotea, akampiga chenga Lakred kabla ya kuujaza wavuni.

Kipindi cha pili, angalau Simba ilionekana kutulia na kusukuma mashambulizi katika lango la Yanga ambao sasa walitegemea zaidi mashambulizi ya kushtukiza.

Alikuwa ni nyota kutoka Ivory Coast, Freddy Michael, aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Saido, aliyepachika bao la kufutia machozi dakika ya 73, akiitendea haki pasi ya Clatous Chama.

Aliwahadaa kwa chenga, Ibrahim hamad 'Bacca' na Bakari Mwamnyeto, kabla ya kuukwamisha wavuni.

Lakred alifanya kazi ya ziada dakika ya 78, alipookoa Simba isifungwe bao la tatu na Kennedy Musonda aliyeingia kuchukua nafasi ya Clement Mzize.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042